# حِصْنُ المُسْلِمِ

## مِنْ أذكارِ الكِتابِ وَالسُّنَّة

### باللغة السواحلية

# Hisn Al-Muslim

## KINGA YA MUISLAMU KATIKA NYIRADI ZA QUR-ANI NA HADITHI ZA MTUME (ﷺ)


Ukusanyaji na Uthibitisho
Said Ali ibn Wahf Al-Qahtaani

Kimefasiriwa na
Shafi Abdur Rahman Omar
Nakuhaririwa na
Abdul Latif Abddul Karim Sheikh
Na kimesahihishwa na
Ziyad Swaleh Lubanga pamoja na
Al-Amini Muhindo Abdul-Rahman.

©Said bin Ali bin Wahaf Al-Qahtani, 1999

King Fahad National Library Cataloging-in-Publication Data

Al-Qahtani, Said bin Ali bin Wahaf
Hisnul Muslim \ translated by Shafi Abdur Rahman Omar - Riyadh
224 p., 8.5 x 12 cm.
ISBN: 9960 - 35 - 442 - 3
(Text in Sawahli)
1. Invocation and awrad    I-Omar, Shafi Abdur Rahman (trans.)
II - Title
212.93 dc    3458/19

Legal Deposit no.: 3458/19
ISBN: 9960 - 35 - 442 - 3

# Ukusanyaji na Uthibitisho

Said Ali ibn Wahf Al-Qahtaani

Kimefasiriwa na

Shafi Abdur Rahman Omar

(kutoka chuo kikuu cha madina)

na kuhaririwa ną

Abdul Latif Abdul Karim Sheikh

(kutoka chuo kikuu cha madina)

Kazi hii imesimamiwa na "ITI"
INVITATION TO ISLAM
Sanduku la Baridi 7325, WALTHAMSTOW, LONDON E17 9TX

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA(Duniani), MWENYE KUREHEMU(Akhera).

## UTANGULIZI:

Hakika sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu,tunamsifu,natunamuomba msaada na tuna muomba maghafira, Mwenyezi Mungu, tunamuomba atuhifadhi na shari za nafsi zetu, na maovu ya matendo yetu, anaemuongoza Mwenyezi Mungu, hapana wakumpoteza, na anaempoteza, hapana wakumuongoza. Nakiri kwamba, hapana apasae kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu, hali ya kuwa peke yake, hana mshirika, na ninakiri kwamba, Muhammad ni mja wake na ni Mtume wake, Mwenyezi Mungu amrehemu na awarehemu jamaa zake na masahaba zake na wanao wafuata hao kwa wema mpaka

siku ya malipo na amsalimishe kwa amani nyingi.

Baada ya yalio tangulia, huu ni ufupi (Mukhtasari) wa kitabu changu kiitwacho “ADHIKRU WA DU’A WA AL-ILAJ BIRRUQAA MINAL-KITAB WA SUNNAH” -(Uradi na Dua na kujitibu kwakutumia Qur’ani, na Hadithi) Nimefupisha humu sehemu ya nyiradi, ili kiwe kitabu hicho, ni chepesi kubebeka safarini, nanimetosheka katika kuthibitisha kusihi nyiradi hizi, kwakutaja vitabu asili viwili au kimoja, na anaetaka maelezo zaidi kuhusu sahaba, basi arejee kwenye asli ya vitabu hivyo.

Ninamuomba Mwenyezi Mungu kwa

majina yake mazuri, na sifa zake zilizo juu, ajaalie kazi hii kuwa, imesafika lengo lake, kwakutaka radhi zake Mwenyezi Mungu Mtukufu, na aninufaishe kwayo katika uhai wangu huu, na baada ya kufa, na amnufaishe atakae kisoma, kukichapisha, au aliekuwa nisababu yakukitawanya, haki yake yeye Mwenyezi Mungu ndie mueza.

Mwenyezi Mungu amrehemu Mtume wetu Muhammad na aali zake na sahaba wake na wanao wafuata hao, kwa wema mpaka siku ya malipo.

❖❖❖

## Fadhila za kumtaja Mwenyezi Mungu

*Amesema Mwenyezi Mungu:*

﴿ فَاذْكُرُونِي أَذْكُرْكُمْ وَاشْكُرُوا لِي وَلاَ تَكْفُرُونِ ﴾

"Nitajeni nami nitawataja, na nishukuruni na wala musinikufuru." ( Suratul Baqarah: 152 )

*Na Akasema:*

﴿ يا أَيُّهَا الَّذِيْنَ آمَنُوا اذْكُرُوْا اللهَ ذِكْرًا كَثِيْرًا ﴾

"Enyi mlioamini mtajeni Mwenyezi Mungu sana." ( Suratul Ahzaab: 41 )

*Akasema tena:*

﴿ وَالذَّاكِرِينَ اللهَ كَثِيرًا وَالذَّاكِرَاتِ أَعَدَّ اللهُ لَهُم مَّغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا ﴾

"Nawasifu wanaume wanaomtaja Mwenyezi Mungu sana na ninawasifu wanawake wanaomtaja

Mwenyezi Mungu kawa andalia wote hao, msamaha na malipo makubwa." (suratul Ahzaab: 35)

*Akasema tena:*

﴿ وَ اذْكُرْ رَبَّكَ فِي نِفسِكَ تَضَرُّعًا وَخِيفَةً وَدُوْنَ الْجَهْرِ
مِنَ الْقَوْلِ بِالْغُدُوِّ وَالآصَالِ وَلا تَكُنْ مِّنَ الْغَافِلِيْنَ ﴾

"Mtaje Mola wako, moyoni mwako kwa unyenyekevu, na kwa uwoga, pasina kudhihirisha sauti, mtaje asubuhi na jioni, nawala usiwe nikatika wenye kughafilika." (Suratul A'raaf 205)

*Mtume ﷺ amesema: 'Mfano wa anaemtaja Mola wake na asie mtaja ni mfano wa alie hai na maiti'.*

*Na akasema ﷺ : "Hivi niwaambieni khabari yamatendo yenu bora, na ambae nimasafi mno, mbele ya mola wenu, na ambae ni ya juu mno katika daraja zenu, na ambae ni bora kwenu kuliko kutoa*

dhahabu, na fedha, na ambae ni bora kuliko kukutana na adui zenu, mkawapiga shingo zao? Wakasema masahaba; Ndio. Akasema Mtume: ﷺ "Nikumtaja Mwenyezi Mungu."

Amesema Mtume ﷺ, Mwenyezi Mungu anasema: 'Mimi niko mbele ya dhana ya mja wangu kwangu, na nipo pamoja nae anapo nitaja, akinitaja moyoni nami ninamtaja moyoni, na akinitaja katika kundi, nami namtaja katika kundi bora zaidi ya hilo lake, na akijikurubisha kwangu paa moja, basi mimi najikurubisha kwake kiasi cha dhiraa, na akijikurubisha kwangu kiasi cha dhiraa, basi mimi nitajikurubisha kwake kiasi chakunyoosha mkono hadi kati ya kifuwa, na akiniijia kwa mwendo mdogo basi nami, nitamjia kwa mwendo wa kasi.

*Imepokewa kutoka kwa Abdallah bin Busr ﷺ kwamba mtu mmoja alisema:*

*"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu; ibada za dini zimekuwa nyingi kwangu, basi nieleze kitu ambacho nitaweza kudumu nacho. Mtume ﷺ akamwambia: "ulimi wako utaendelea kuwa rutuba (yaani sio ukavu), kwakumtaja Mwenyezi Mungu.*

*Na amesema tena Mtume ﷺ: 'Anaesoma harufu moja katika kitabu cha Mwenyezi Mungu basi anapata thawabu za jema moja, na jema ni kwa mema kumi, si semi kuwa "Alif laam miim" ni harufu moja lakini ni kwamba "Alif " peke yake ni harufu moja, na "Laam" ni harufu, na "Miim" ni harufu*

*Imepokewa kutoka kwa Uqbah bin Aamir ﷺ amesema: 'Ametoka Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na sisi tuko sehemu*

*iitwayo Assufah, akasema: "Nani kati yenu anapenda aende kila siku sehemu iitwayo But-haan au Aqiq aje na ngamia wawili walio nenepa pasi na dhambi wala kukata undugu ? " wakasema maswahaba: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu tunapenda hivyo', akasema Mtume; "Hivi haende (asubuhi) mmoja wenu mskitini, akajuwa, au akasoma Aya mbili, za kitabu cha Mwenyezi Mungu?*

*Hizo Aya mbili ni bora kwake kuliko kupata ngamia wawili, na endapo atasoma Aya tatu zita kuwa ni bora kwake kuliko ngamia watatu, na Aya nne ni bora kwake kuliko ngamia wanne, na vilevile zaidi ya hapo Aya zozote atakazo zisoma basi ni bora kwake kuliko hisabu yake kwa ngamia."*

*Na amesema Mtume ﷺ: 'Anae kaa kikao chochote kile asimtaje Mwenyezi Mungu*

*katika kikao hicho basi ana dhambi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na anae lala sehemu yoyote ile kisha asimtaje Mwenyezi Mungu wakati wakuinuka sehemu hiyo basi ana dhambi kwa Mwenyezi Mungu'.*

*Amesema Mtume:* ﷺ *"Hapana watu wowote wale, wanao simama katika kikao walicho kaa, kisha wasimtaje Mwenyezi Mungu, ila watakuwa wana simama kama mwenye kuukimbia, mzoga wa punda, na wata kuja juta kwa kutomtaja Mwanyezi Mungu.*

*Amesema Mtume* ﷺ*: 'Hapana watu wowote wale wanao simama katika kikao walicho kaa, kisha wasimtaje Mwenyezi Mungu ila watakuwa wanasimama kama mzoga wa punda, na watakuja juta kwa kutomtaja Mwenyezi Mungu'.*

**1. Dua za kuamka kutoka usingizini.**

(١) الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَحْيَانَا بَعْدَ مَا أَمَاتَنَا وإِلَيْهِ النُّشُوْرُ .

"Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu ambae ametupa uhui baada ya kutufisha na ni kwake tu kufufuliwa."

*Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ:*

'Mwenye Kushutuka usingizini usiku akasema:

(٢) لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ لاَشَرِيكَ لَهُ ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ، سُبْحَانَ اللَّهِ ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ ، وَلاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ وَلاَحَوْلَ وَلاَ قُوَّةَ إِلاَّ بِاللَّهِ

الْعَلِيِّ الْعَظِيمِ ، رَبِّ اغْفِرْ لِي .

"Hapana mola, apasae kuabudiwa kwa haki ila mwenyezi mungu, hali yakuwa peke yake hana mshirika, ni wake ufalme, na ni zake sifa njema, na yeye juu ya kila kitu ni muweza, ametakasika mwenyezi mungu, na sifa njema zote ni zake, na hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila ni mwenyezi mungu, na Mwenyezi Mungu ni mkubwa, na hapana uwezo wala nguvu, isipokuwa vyote vinatokana na Mwenyezi Mungu, alie juu, alie mtukufu, ewe Mola(Mwenyezi Mungu); nisamehe."

*.....basi atasamehewa. Na kama atasimama akaenda kutawadha, akaswali, basi swala yake atakubaliwa.*

(٣) الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي عَافَانِي فِي جَسَدِي وَرَدَّ عَلَيَّ رُوحِي وأَذِنَ لِي بِذِكْرِهِ .

"Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu ambae amenipa uzima wa mwili wangu, na akanirudishia roho yangu, na akaniruhusu kumtaja."

(٤) ﴿ إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمٰوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلٰفِ الَّيْلِ وَالنَّهَارِ لَأَيٰتٍ لِأُولِى الْأَلْبٰبِ ..... ﴾ .

(سورة آل عمران: ١٩٠- ٢٠٠)

**2. Dua ya kuvaa nguo.**

(٥) الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي كَسَانِي هَذَا (الثَّوْبَ) وَرَزَقَنِيهِ مِنْ غَيْرِ حَوْلٍ مِنِّي وَلَا قُوَّةٍ .

"Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu ambae amenivisha nguo hii, na kuniruzuku pasina uwezo kutoka kwangu wala nguvu."

**3. Dua ya kuvaa nguo mpya .**

(٦) اللَّهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ أَنْتَ كَسَوْتَنِيهِ أَسْأَلُكَ مِنْ خَيْرِهِ وَخَيْرِ مَا صُنِعَ لَهُ ، وأَعُوْذُ بِكَ مِنْ شَرِّهِ وَشَّرِ مَا صُنِعَ لَهُ .

"Ewe Mwenyezi Mungu, sifa njema ni zako, wewe ndie ulienivisha, nakuomba kheri ya nguo hii, na kheri ya kila ambacho nguo hii, imetengenezewa, na najilinda kwako kutokamana na shari yake, na shari ambayo nguo hii imetengenezewa."

**4. Dua unayo muombea aliyevaa nguo mpya.**

(٧) تُبْلِى وِيُخْلِفُ اللَّهُ تَعَالَى .

"Itakwisha (kwa kuzeeka na kupasuka)

na Mwenyezi Mungu atakupa nyingine."

(٨) اِلْبَسْ جَدِيداً وَعِشْ حَمِيداً وَمُتْ شَهِيداً .

"Vaa nguo mpya, na ishi hali ya kuwa ni mwenye kushukuru, na kufa hali ya kuwa ni shahidi."

**5. Dua ya kuvua nguo.**

(٩) بِسْمِ اللّٰهِ .

"Kwa jina la MwenyeziMungu(nina vua)."

**6. Dua ya kuingia chooni.**

(١٠) [بِسْمِ اللّٰهِ] اللّٰهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْخُبُثِ وَالْخَبَائِثِ .

"(Kwa jina la Mwenyezi Mungu), Ewe Mwenyezi Mungu najilinda kwako kutokana na mashetani ya kiume na ya kike."

**7. Dua ya kutoka chooni.**

(١١) غُفْرَانَكَ .

"Nakuomba msamaha (Ewe Mwenyezi Mungu)."

**8. Dua ya kabla ya kutawadha.**

(١٢) بِسْمِ اللَّهِ .

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu (nina tawadha)."

**9. Dua baada ya kutawadha.**

(١٣) أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ

لاَشَـرِيكَ لَـهُ وَأَشْـهَدُ أَنَّ مُحَمَّـداً عَبْـدُهُ وَرَسُوْلُهُ .

"Nakiri kwa moyo na kusema kwa ulimi kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mwenyezi Mungu, peke yake, wala hana mshirika wake, na ninakiri kwamba Muhammad ﷺ ni mja wake na ni mtume wake."

(١٤) اللَّهُمَّ اجْعَلْنِي مِـنَ التَّوَّابِـينَ وَاجْعَلْنِـي مِنَ الْمُتَطَهِّرِينَ .

"Ewe Mwenyezi Mungu nijaalie niwe miongoni mwa wale wanaoomba msamaha, na nijaalie miongoni mwa wale walio safi."

(١٥) سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْـدِكَ أَشْـهَدُ أَنْ

لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ أَسْتَغْفِرُكَ وَأَتُوْبُ إِلَيكَ .

"Utakatifu ni wako, Ewe Mola wangu, na shukrani zote zina rudi kwako, nakiri kwamba hapana apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Wewe, naomba msamaha wako, nanarejea kwako (kwaku tubia)".

**10. Dua ya kutoka nyumbani.**

(١٦) بِسْمِ اللَّهِ تَوَكَّلْتُ عَلَى اللَّهِ وَلاَحَوْلَ وَلاَقُوَّةَ إِلاَّ بِاللَّهِ .

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu (ninatoka), ninamtegemea Mwenyezi Mungu, na hapana uwezo wala nguvu ila vyote vinatokana na Mwenyezi Mungu."

(١٧) اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوْذُ بِكَ أَنْ أَضِلَّ ، أَوْ أُضَلَّ ، أَوْ أَزِلَّ ، أَوْ أُزَلَّ أَوْ أَظْلِمَ أَوْ أُظْلَمَ ،

أَوْ أَجْهَلَ ، أَوْ يُجْهَلَ عَلَيَّ .

"Ewe Mwenyezi Mungu najilinda kwako kutokamana na kupotea au kupoteza, au kuteleza, au kumtelezesha mtu, au kudhulumu au kudhulumiwa, au kuwa mjinga au kufanywa mjinga."

**11. Dua ya kuingia nyumbani.**

(١٨) بِسْمِ اللَّهِ وَلَجْنَا ، وَبِسْمِ اللَّهِ خَرَجْنَا ، وَعَلَى رَبِّنَا تَوَكَّلْنَا .

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu tuna ingia, na kwa jina la Mwenyezi Mungu tuna toka, na Mola wetu tunamtegemea."

*Kisha asalimie watu walio ndani:*

**12. Dua ya kwenda Msikitini.**

(١٩) اللَّهُمَّ اجْعَلْ فِي قَلْبِي نُوْراً ، وَفِي

لِسَانِي نُوْراً ، وَفِي سَمْعِي نُوْراً ، وَفِي بَصَرِي نُوْراً ، وَمِنْ فَوْقِي نُوْراً ، وَمِنْ تَحْتِي نُوْراً ، وَعَنْ يَمِينِي نُوْرًا ، وَعَنْ شِمَالِي نُوْراً ، وَمِنْ أَمَامِي نُوْراً ، وَمِنْ خَلْفِي نُوْراً ، وَاجْعَلْ فِي نَفْسِي نُوْراً ، وَأَعْظِمْ لِي نُوْراً ، وَعَظِّمْ لِي نُوْراً ، وَاجْعَلْ لِي نُوْراً ، وَاجْعَلْنِي نُوْراً ، اللَّهُمَّ أَعْطِنِي نُوْراً ، وَاجْعَلْ فِي عَصَبِي نُوْراً ، وَفِي لَحْمِي نُوْراً ، وَفِي دَمِي نُوْراً ، وَفِي شَعْرِي نُوْراً ، وَفِي بَشَرِي نُوْراً . [اللَّهُمَّ اجْعَلْ لِي نُوْراً فِي قَبْرِي .. وَنُوْرًا فِي عِظَامِي] [وَزِدْنِي نُوْرًا ،

وَزِدْنِي نُوْرًا ، وَزِدْنِـي نُـوْرًا ] [وَهَـبْ لِـي نُوْرًا عَلَى نُوْرًا ] .

"Ewe Mwenyezi Mungu, weka katika moyo wangu nuru, na katika ulimi wangu nuru, na katika maskio yangu nuru, na katika macho yangu nuru, na ju yangu nuru, na chini yangu nuru, na kuliani kwangu nuru, na kushotoni kwangu nuru, na mbele yangu nuru, na nyuma yangu nuru, na weka katika nafsi yangu nuru, na nifanyie kubwa nuru, na nifanyie nyingi nuru, nauniwekee mimi nuru, na unifanye mimi nuru, Ewe Mwenyezi Mungu nipe nuru, na uweke katika mishipa yangu nuru, na katika nyama yangu nuru, nakatika damu yangu nuru, na katika nywele zangu nuru, na katika ngozi yangu nuru, [Ewe Mwenyezi Mungu niwekee nuru katika kaburi

ya ngu, na nuru katika mifupa yangu ] [na unizidishe nuru, na unizidishe nuru, na unizidishe nuru] [na unipe nuru juu ya nuru] .

**13. Dua ya kuingia Msikitini.**

(٢٠) أَعُوْذُ بِاللّٰهِ الْعَظِيمِ وَبِوَجْهِهِ الْكَرِيمِ ، وَسُلْطَانِهِ الْقَدِيمِ ، مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ، [بِسْمِ اللّٰهِ ، وَالصَّلاَةُ] [وَالسَّلاَمُ عَلَى رَسُوْلِ اللّٰهِ] ، اللّٰهُمَّ افْتَحْ لِي أَبْوَابَ رَحْمَتِكَ

"Najilinda na Mwenyezi Mungu aliye Mtukufu, na kwa uso wake mtakatifu, na kwa utawala wake wa kale, kutokana na shetani aliyeepushwa na rehma za Mwenyezi Mungu, (kwa jina la mwenyezi mungu, na rehma), (na amani zimfikie mtume wa mwenyezi mungu),

Ewe mwenyezi mungu nifunguliye milango ya rehema zako" .

**14. Dua ya kutoka Msikitini.**

(٢١) بِسْــمِ اللّٰـهِ وَالصَّــلاَةُ وَالسَّــلاَمُ عَلَــى رَسُوْلِ اللّٰهِ ، اللّٰهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ مِنْ فَضْلِكَ ، اللّٰهُمَّ اعْصِمْنِي مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ .

"Kwa Jina la Mwenyezi Mungu na rehema na amani zimfikie Mtume wa Mwenyezi Mungu, Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nakuomba katika fadhila zako, Ewe Mwenyezi Mungu nilinde kutokana na shetani aliyeepushwa na rehma zako(aliye laaniwa)

**15. Dua za Adhan.**

*Mtu akisikia Muadhini anaadhini anatakiwa aseme kama anavyo sema*

*Muadhini, ila atakapo sema:*

(٢٢) حَيَّ عَلَى الصَّلاةِ

'Hayya ala swalaah'

"Njooni kwenye swala."

حَيَّ عَلَى الْفَلاحِ

'Hayya alal falaah'.

"Njooni kwenye mafanikio."

*yeye hato muigiza, bali anatakiwa aseme*:

لاَحَوْلَ وَلاَقُوَّةَ إِلاَّ بِاللَّهِ

'Laa Haula walaa quwwata illaa billah.'

"Hapana uwezo wala nguvu ila za Mwenyezi Mungu."

*Muadhini akisema;* Ash-hadu anla ilaha

illa Laah, ash-hadu anna Muhammada Rrasuulu Laah,

*Anatakiwa mtu aseme*:

(٢٣) وَأَنَا أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ لاَشَرِيكَ لَهُ وَأَنَّ مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُوْلُهُ ، رَضِيتُ بِاللَّهِ رَبًّا ، وَبِمُحَمَّدٍ رَسُوْلاً ، وَبِالإِسْلاَمِ دِيناً .

"Na mimi pia nakiri kwa moyo, na kusema kwa ulimi, kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki, ila mwenyezi mungu Mmoja peke yake, hana mushrika wake, na kwamba Muhammad ni mja wake, na ni mtume wake,nimeridhia kuwa Mwenyezi Mungu ndie bwana wangu, na kuwa Muhammad ni Mtume wangu, na kuwa

Uislamu ndio dini yangu."

*(24) Kisha baada ya kumjibu Muadhini atamswalia Mtume ﷺ.*

*Kisha atasema:*

(٢٥) اللَّهُمَّ رَبَّ هَذِهِ الدَّعْوَةِ التَّامَّةِ ، وَالصَّلاةِ القَائِمَةِ ، آتِ مُحَمَّداً الْوَسِيلَةَ وَالْفَضِيلَةَ ، وَابْعَثْهُ مَقَاماً مَحْمُوْداً الَّذِي وَعَدْتَهُ ، [إِنَّكَ لاَ تُخْلِفُ الْمِيعَادِ] .

"Ewe Mwenyezi Mungu, bwana wa mlingano(mwito) huu uliotimia, na sala ilio simama, mpe (Mtume) Muhammad Wasila, na fadhila, na mfikishe daraja yenye kusifiwa, ambayo umemuahidi, (kwani wewe hukhalifu ahadi)" .

*(26) Inafaa kwa mtu kujiombea kati ya Adhana na Iqamah, kwani dua kati ya*

*Adhana na Iqamah hairudishwi.*

**16. Dua za kufungulia Salah.**

(٢٧) اللَّهُمَّ بَاعِدْ بَيْنِي وَبَيْنَ خَطَايَايَ كَمَا بَاعَدْتَ بَيْنَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ ، اللَّهُمَّ نَقِّنِي مِنْ خَطَايَايَ ، كَمَا يُنَقَّى الثَّوْبُ الأَبْيَضُ مِنَ الدَّنَسِ ، اللَّهُمَّ اغْسِلْنِي مِنْ خَطَايَايَ ، بِالثَّلْجِ وَالْمَاءِ وَالْبَرْدِ .

"Ewe Mwenyezi Mungu niweke mbali na madhambi yangu kama ulivyoweka mbali baina ya mashariki na magharibi, Ewe Mwenyezi Mungu nitakase na madhambi yangu kama vile inavyo takaswa nguo nyeupe na uchafu, Ewe Mwenyezi Mungu nisafishe na madhambi yangu kwa theluji na kwa maji na kwa barafu."

(٢٨) سُبْحَانَكَ اللَّهُــمَّ وَبِحَمْـدِكَ ، وَتَبَـارَكَ اسْمُكَ ، وَتَعَالَى جَدُّكَ ، وَلاَ إِلَهَ غَيْرُكَ .

"Kutakasika ni kwako, ewe Mwenyezi Mungu, na sifa njema zote ni zako, na limetukuka jina lako, na utukufu niwako, na hapana apasae kuabudiwa kwa haki, asie kuwa Wewe.

(٢٩) وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضَ حَنِيفاً وَمَا أَنَا مِـنَ الْمُشْـرِكِينَ ، إِنَّ صَلاتِي ، وَنُسُكِي ، وَمَحْيَايَ ، وَمَمَاتِي لِلَّــهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ، لاَ شَرِيكَ لَهُ وَبِذَالِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا مِنَ الْمُسْلِمِينَ. اللَّهُمَّ أَنْتَ الْمَلِكُ لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ. أَنْــتَ رَبِّـي وَأَنَـا عَبْـدُكَ ، ظَلَمْـتُ

نَفْسِي وَاعْتَرَفْتُ بِذَنْبِي فَاغْفِرْ لِي ذُنُوبِي جَمِيعاً إِنَّهُ لاَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلاَّ أَنْتَ. وَاهْدِنِي لأَحْسَنِ الأَخْلاقِ لاَ يَهْدِي لأَحْسَنِهَا إِلاَّ أَنْتَ ، وَاصْرِفْ عَنِّي سَيِّئَهَا ، لاَ يَصْرِفُ عَنِّي سَيِّئَهَا إِلاَّ أَنْتَ ، لَبَّيْكَ وَسَعْدَيْكَ ، وَالْخَيْرُ كُلُّهُ بِيَدَيْكَ ، وَالشَّرُّ لَيْسَ إِلَيْكَ، أَنَا بِكَ وَإِلَيْكَ ، تَبَارَكْتَ وَتَعَالَيْتَ ، أَسْتَغْفِرُكَ وَأَتُوبُ إِلَيْكَ .

"Nimeuelekeza uso wangu kwa yule ambae ameumba mbingu na ardhi hali ya kumtakasia yeye dini yangu, na sikuwa mimi ni katika washirikina, hakika swala yangu na kuchinja kwangu na uhai

wangu, na kufa kwangu ni kwa Mwenyezi Mungu Bwana wa viumbe vyote, hana mshirika, na kwa hilo nime amrishwa, nami ni katika waislamu, Ewe munyezi mungu, wewe ndie mfalme, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila wewe, wewe ndie bwana wangu na mimi ni mtumwa (mja) wako, nimeidhulumu nafsi yangu, na nimekiri madhambi yangu kwa hivyo nisamahe madhambi yangu yote, hakika hasamehe madhambi, ila Wewe. Na niongoze kwenye tabia njema (nzuri), kwani haongoze kwenye tabia nzuri, ila Wewe, niepushe na tabia mbaya, kwani hakuna mwenye uwezo wakuniepusha na tabia mbaya, ila Wewe, naitikia mwito wako, naninafuraha kukutumikia, na kheri zote ziko mikononi mwako, na shari haitoki kwako, mimi nimepatikana kwa ajili yako, na nitarudi kwako, umetakasika,

na umetukuka, nakutaka msamaha naninarejea kwako (kwa kutubia)".

(٣٠) اللَّهُمَّ رَبَّ جِبْرَائِيلَ ، وَمِيكَائِيلَ ، وَإِسْرَافِيلَ فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضَ ، عَالِمَ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ ، أَنْتَ تَحْكُمُ بَيْنَ عِبَادِكَ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ. اِهْدِنِي لِمَا اخْتُلِفَ فِيهِ مِنَ الْحَقِّ بِإِذْنِكَ إِنَّكَ تَهْدِي مَنْ تَشَاءُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ .

"Ewe Mwenyezi Mungu, Mola wa Jibriil na Miikaail na Israafil, Muumba wa mbingu na ardhi, Mjuzi wa mambo yaliojificha na yaliowazi, Wewe unahukumu baina ya waja wako katika mambo ambayo walikuwa wakitafautiana, niongoze mimi kwenye

haki katika yale waliotafautiana kwa ruhusa yako, hakika Wewe unamuongoza umtakae kwenye njia ilionyoka.”

(٣١) اللَّهُ أَكْبَرُ كَبِيراً ، اللَّهُ أَكْبَرُ كَبِيراً ، اللَّهُ أَكْبَرُ كَبِيراً ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ كَثِيراً ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ كَثِيراً ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ كَثِيراً ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ كَثِيراً ، وَسُبْحَانَ اللَّهِ بُكْرَةً وَأَصِيلاً . ( ثلاثاً )

أَعُوْذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ مِنْ نَفْخِهِ وَنَفْثِهِ وَهَمْزِهِ .

"Mwenyezi Mungu ni Mkubwa, Mwenyezi Mungu ni Mkubwa, Mwenyezi Mungu ni Mkubwa, sifa

njema niza mwenyezi mungu, kwa wingi na sifa njema ni za mwenyezi mungu, kwa wingi, na sifa njema ni za mwenyezi Mungu kwa wingi, na ametakasika Mwenyezi Mungu asubuhi na jioni."

(Atasema haya mara tatu).

"Najilinda na Mwenyezi Mungu kutokana na shetani, na kupulizia kwake, na kutabana kwake na kutia kwake wasiwasi katika nyoyo za binadamu."

*Mtume ﷺ alikuwa akiamka usiku, ili kufanya ibada anasema:*

(٣٢) اللَّهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ أَنْتَ نُورُ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضِ وَمَنْ فِيهِنَّ ، وَلَكَ الْحَمْدُ أَنْتَ قَيِّمُ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضِ وَمَنْ فِيهِنَّ ، ] وَلَكَ الْحَمْدُ أَنْتَ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضِ وَمَنْ

فِيهِنَّ ] [ وَلَكَ الْحَمْدُ لَكَ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضِ وَمَنْ فِيهِنَّ ] [ وَلَكَ الْحَمْدُ أَنْتَ مَلِكُ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضِ ] [ وَلَكَ الْحَمْدُ ] [أَنْتَ الْحَقُّ ، وَوَعْدُكَ الْحَقُّ ، وَقَوْلُكَ الْحَقُّ ، وَلِقَاؤُكَ الْحَقُّ ، وَالْجَنَّةُ حَقٌّ، وَالنَّارُ حَقٌّ ، وَالنَّبِيُّونَ حَقٌّ ، وَمُحَمَّدٌ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَ سَلَّمْ حَقٌّ ، وَالسَّاعَةُ حَقٌّ ] [ اللَّهُمَّ لَكَ أَسْلَمْتُ ، وَعَلَيْكَ تَوَكَّلْتُ، وَبِكَ آمَنْتُ، وَإِلَيْكَ أَنَبْتُ وَبِكَ خَاصَمْتُ وَإِلَيْكَ حَاكَمْتُ. فَاغْفِرْ لِى مَا قَدَّمْتُ ، وَمَا أَخَّرْتُ، وَمَا أَسْرَرْتُ ، وَمَا أَعْلَنْتُ ] [ أَنْتَ

الْمُقَدِّمُ ، وَأَنْتَ الْمُؤَخِّرُ ، لاَ إِلَـهَ إِلاَّ أَنْـتَ ]

أَنْتَ إِلَهِي لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنتَ ] .]

"Ewe Mwenyezi Mungu nizako sifa njema, Wewe ndie nuru ya mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake; na nizako sifa njema, Wewe ndie sababu ya kusimama kwa mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake; na nizako sifa njema, Wewe ndiwe Mola wa mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake; na nizako sifa njema, ni wako Ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake; na nizako sifa njema, Wewe ndiwe Mfalme wa mbingu na ardhi, na nizako sifa njema, Wewe ni Haki (kweli), na ahadi yako ni yakweli, na neno lako ni lakweli, na kukutana na Wewe ni kweli, na pepo ni kweli, na moto ni kweli, na Mitume ni

kweli, na Muhammad ﷺ ni kweli, na Qiyama ni kweli, Ewe Mwenyezi Mungu, kwako nime jisalimisha, na kwako nime tegemea, nawewe nime kuamini, na kwako nimeregea, na kwa ajili yako nimeteta, na kwako nimehukumu, kwa hivyo nisamehe niliyo yatanguliza, na niliyo yachelewesha, na niliyo yaficha na niliyo yatangaza; Wewe ndie mwenye kutanguliza na Wewe ndie mwenye kucheleweshа, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe; Wewe ndie Mola wangu, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe."

## 17. Dua ya wakati wa kurukuu

(٣٣) سُبْحَانَ رَبِّيَ الْعَظِيمِ . (ثلاثًا)

"Ametakasika Mola wangu,aliye Mtukufu."

(Utasema mara tatu).

(٣٤) سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ رَبَّنَا وَبِحَمْدِكَ اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِيْ .

"Kutakasika ni kwako, Ewe Mwenyezi Mungu, Mola wetu, na sifa njema zote ni zako ewe Mwenyezi Mungu, nisamehe"

(٣٥) سُبُّوحٌ قُدُّوسٌ رَبُّ الْمَلائِكَةِ وَالرُّوحِ .

"Mwingi wa kutakaswa, Mtakatifu, Mola wa malaika na Jibriil."

(٣٦) اللَّهُمَّ لَكَ رَكَعْتُ ، وَبِكَ آمَنْتُ ، وَلَكَ أَسْلَمْتُ خَشَعَ لَكَ سَمْعِي ، وَبَصَرِي ، وَمُخِّي ، وَعَظْمِي وَعَصَبِي ، وَمَا اسْتَقَلَّ بِهِ قَدَمِي .

"Ewe Mwenyezi Mungu kwako nimerukuu, na Wewe nimekuamini, na kwako nimejisalimisha, umenyenyekea kwako usikizi wangu, na uwoni wangu, na ubongo wangu, na mfupa wangu, na hisia zangu, na ambacho kimesimama juu ya miguu yangu."

(٣٧) سُــــبْحَانَ ذِي الْجَــــــبَرُوتِ ، وَالْمَلَكُوتِ ، وَالْكِبْرِيَاءِ ، وَالْعَظَمَةِ .

"Ametakasika Mwenye Utawala, na Ufalme, na Ukubwa, na Utukufu."

**18. Dua ya kuinuka kutoka kwenye rukuu.**

(٣٨) سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ .

"Mwenyezi Mungu amemsikia mwenye kumsifu."

(٣٩) رَبَّنَا وَلَكَ الْحَمْدُ ، حَمْداً كَثِيراً طَيِّباً مُبَارَكاً فِيهِ .

"Ewe Bwana wetu ni zako sifa njema, sifa nyingi, nzuri, zenye baraka."

(٤٠) مِلْءَ السَّمَوَاتِ وَمِلْءَ الأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ، وَمِلْءَ مَا شِئْتَ مِنْ شَيْءٍ بَعْدُ. أَهْلَ الثَّنَاءِ وَالْمَجْدِ ، أَحَقُّ مَا قَالَ الْعَبْدُ، وَكُلُّنَا لَكَ عَبْدٌ. اللَّهُمَّ لاَ مَانِعَ لِمَا أَعْطَيْتَ، وَلاَ مُعْطِيَ لِمَا مَنَعْتَ ، وَلاَ يَنْفَعُ ذَا الْجَدِّ مِنْكَ الْجَدُّ .

"Zimejaa mbingu, na zimejaa ardhi, navili vyomo ndani yake sifa zako, nazimejaa (sifa zako) kwa ulicho kitaka

baada yake, Wewe ni mstahiki wa sifa na utukufu, ni kweli aliyo yasema mja wako, na sote ni waja wako, Ewe Mwenyezi Mungu hapana anaeweza kukizuia ulichokitoa, na wala kutoa ulichokizuia, na wala haumnufaishi mwenye utajiri, kwani kwako Wewe ndio utajiri."

**19. Dua ya wakati wa kusujudu.**

(٤١) سُبْحَانَ رَبِّيَ الأَعْلَى (ثلاثًا).

"Ametakasika Mola wangu aliyejuu."

(atasema hivi mara tatu)

(٤٢) سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ رَبَّنَا وبِحَمْدِكَ اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي.

"Kutakasika ni kwako, Ewe Mwenyezi Mungu, Mola wetu, na sifa njema zote ni zako, Ewe Mwenyezi Mungu nisamehe."

(٤٣) سُبُّوحٌ قُدُّوسٌ رَبُّ الْمَلائِكَةِ وَالـرُّوحِ

"Mwingi wa kutakaswa, Mtakatifu, Mola wa malaika na Jibriil."

(٤٤) اللَّهُـمَّ لَـكَ سَـجَدْتُ وَبِـكَ آمَنْـتُ ، وَلَكَ أَسْلَمْتُ ، سَجَدَ وَجْهِيَ لِلَّذِي خَلَقَـهُ ، وَصَوَّرَهُ ، وَشَقَّ سَمْعَهُ وَبَصَرَهُ ، تَبَارَكَ اللَّـهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ .

"Ewe Mwenyezi Mungu kwako nimesujudu, na Wewe nimekuamini, na kwako nimesilimu, umesujudu uso wangu kumsujudia aliyeuumba na akautia sura na akaupasua usikizi wake na uwoni wake, ametukuka Mwenyezi Mungu, Mbora wa waumbaji."

(٤٥) سُبْحَانَ ذِي الْجَبَرُوتِ ، وَالْمَلَكُوتِ ، وَالْكِبْرِيَاءِ ، وَالْعَظَمَةِ .

"Ametakasika Mwenye Utawala, na Ufalme, na Ukubwa, na Utukufu."

(٤٦) اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي ذَنْبِي كُلَّهُ ، دِقَّهُ وَجِلَّهُ ، وَأَوَّلَهُ وَآخِرَهُ وَعَلانِيَتَهُ وَسِرَّهُ .

"Ewe Mwenyezi Mungu nisamehe dhambi zangu zote, ndogo na kubwa, za mwanzo na za mwisho, za dhahiri na za siri."

(٤٧) اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِرِضَاكَ مِنْ سَخَطِكَ ، وَبِمُعَافَاتِكَ مِنْ عُقُوبَتِكَ ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْكَ ، لاَ أُحْصِي ثَنَاءً عَلَيْكَ أَنْتَ كَمَا أَثْنَيْتَ عَلَى نَفْسِكَ .

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi najilinda kwa radhi zako kutokana na hasira zako, na kwa msamaha wako kutokana na adhabu yako, na najilinda kwako unihifadhi na Wewe, mimi siwezi kuzidhibiti sifa zako, Wewe ni kama ulivyojisifu Mwenyewe."

**20. Dua za kikao kati ya sijda mbili.**

(٤٨) رَبِّ اغْفِرْ لِي ، رَبِّ اغْفِرْ لِي .

"Mola nisamehe, Mola nisamehe."

(٤٩) اللَّهُـــمَّ اغْفِـــرْ لِـــي ، وَارْحَمْنِـــي ، وَاهْدِنِي ، وَاجْـبُرْنِي ، وَعَـافِنِي ، وَارْزُقْنِـي ، وَارْفَعْنِي .

"Ewe Mwenyezi Mungu nisamehe, na

unirehemu, na uniongoze, na uniungie, na unipe afya, na uniruzuku na uniinue.”

**21. Dua za sijda ya kisomo.**

(٥٠) سَجَدَ وَجْهِيَ لِلَّذِي خَلَقَهُ ، وَشَقَّ سَمْعَهُ وَبَصَرَهُ بِحَوْلِهِ وَقُوَّتِهِ ، ﴿فَتَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ﴾

"Umesujudu uso wangu kumsujudia yule ambae ameuumba na akapasuwa masikio yake, na macho yake, kwa uwezo wake na nguvu zake, {{Ametukuka Mwenyezi Mungu mbora wa waumbaji}}.”

(٥١) اللَّهُمَّ اكْتُبْ لِي بِهَا عِنْدَكَ أَجْراً ، وَضَعْ عَنِّي بِهَا وِزْراً ، وَاجْعَلْهَا لِي عِنْدَكَ ذُخْراً ، وَتَقَبَّلْهَا مِنِّي كَمَا تَقَبَّلْتَهَا مِنْ عَبْدِكَ دَاوُدَ .

“Ewe Mwenyezi Mungu niandikie kwako kwa sijda hii malipo, na nifutie kwayo madhambi, na ijaalie kwangu mbele yako ni akiba, na nikubalie kama ulivyo mkubalia mja wako Dawud.”

### 22. Dua ya Tashahhud

(٥٢) التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ ، وَالصَّلَوَاتُ ، وَالطَّيِّبَاتُ ، السَّلاَمُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ ، السَّلاَمُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ. أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ .

"Maamkuzi mema, na rehema na mazuri yote, ni kwa Mwenyezi Mungu, amani

zishuke juu yako Ewe Mtume, na rehema za Mwenyezi Mungu na baraka zake, amani ishuke juu yetu, na juu ya waja wa Mwenyezi Mungu walio wema, nakiri kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mwenyezi Mungu, na ninakiri kwamba Muhammad ni mja wake na ni mtume wake."

**23. Kumsalia Mtume ﷺ baada ya tashahhud.**

(٥٣) اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ، اللَّهُمَّ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ.

"Ewe Mwenyezi Mungu mrehemu Muhammad na jamaa zake Muhammad, kama ulivyo mrehemu Ibrahim, na jamaa zake Ibrahim, hakika Wewe ni Mwenye kusifika Mtukufu, Ewe Mwenyezi Mungu mbariki Muhammad na jamaa zake Muhammad, kama ulivyo mbariki Ibrahim na jamaa zake Ibrahim, hakika Wewe ni Mwenye kusifika Mtukufu."

(٥٤) اللّٰهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى أَزْوَاجِهِ وَذُرِّيَّتِهِ ، كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ. وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى أَزْوَاجِهِ وَذُرِّيَّتِهِ ، كَمَا بَارَكْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ .

"Ewe Mwenyezi Mungu mrehemu Muhammad, na wake zake, na kizazi

chake, kama ulivyo warehemu jamaa wa Ibrahim. Na mbariki Muhammad, na wake zake, na kizazi chake, kama ulivyo wabariki jamaa zake Ibrahim, hakika Wewe Umesifika na Umetukuka."

**24. Dua baada ya Tashahhud.**

(٥٥) اللَّهُـمَّ إِنِّـي أَعُـوْذُ بِـكَ مِـــنْ عَــذَابِ الْقَبْرِ ، وَمِنْ عَذَابِ جَهَنَّمَ ، وَمِنْ فِتْنَةِ الْمَحْيَا وَالْمَمَاتِ ، وَمِنْ شَرِّ فِتْنَةِ الْمَسِيحِ الدَّجَّالِ .

"Ewe Mwenyezi Mungu mimi nakutaka unihifadhi na adhabu ya kaburi, na adhabu ya (moto wa) jahannam, na fitna ya uhai, na ya kufa, na shari ya fitna ya Masihi-ddajjal"

(٥٦) اللَّهُـمَّ إِنِّـي أَعُـوْذُ بِـكَ مِـــنْ عَــذَابِ

الْقَبْرِ ، وأَعُوْذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ الْمَسِيحِ الدَّجَّالِ ، وأَعُوْذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ الْمَحْيَا وَالْمَمَاتِ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوْذُ بِكَ مِنَ الْمَأْثَمِ وَالْمَغْرَمِ .

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi najilinda kwako kutokana na adhabu ya kaburi, na najilinda kwako kutokana na fitna ya Masihi-dajal, na najilinda kwako kutokana na fitna ya uhai na ya mauti, Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi najilinda kwako kutokana na dhambi na deni."

(٥٧) اللَّهُمَّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي ظُلْماً كَثِيراً ، وَلاَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلاَ أَنْتَ ، فَاغْفِرْ لِي مَغْفِرَةً مِنْ عِنْدِكَ وَارْحَمْنِي إِنَّكَ أَنْتَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ .

“Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi nime idhulumu nafsi yangu, dhulma kubwa, na hasamehe madhambi ila Wewe, basi nisamehe msamaha kutoka kwako, na unirehemu, hakika Wewe ni mwingi wa kusamehe, mwingi wa kurehemu.”

(٥٨) اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي مَا قَدَّمْتُ ، وَمَا أَخَّرْتُ ، وَمَا أَسْرَرْتُ ، وَمَا أَعْلَنْتُ ، وَمَا أَسْرَفْتُ ، وَمَا أَنْتَ أَعْلَمُ بِهِ مِنِّي. أَنْتَ الْمُقَدِّمُ ، وَأَنْتَ الْمُؤَخِّرُ لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ .

"Ewe Mwenyezi Mungu ni samehe niliyo ya tanguliza, na niliyo ya chelewesha, na niliyo ya fanya kisiri na niliyo ya fanya kwa dhahiri, na niliyo ruka mipaka, na ambayo Wewe unayajua

zaidi kuliko mimi, Wewe ndiwe mwenye kutanguliza, na Wewe ndiwe mwenye kucheleweshа, hakuna apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe."

(٥٩) اللَّهُمَّ أَعِنِّي عَلَى ذِكْرِكَ ، وَشُكْرِكَ ، وَحُسْنِ عِبَادَتِكَ .

"Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie kukukumbuka, na kukushukuru, na uzuri wa kukuabudu."

(٦٠) اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْبُخْلِ ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الْجُبْنِ ، وأَعُوذُ بِكَ مِنْ أَنْ أُرَدَّ إِلَى أَرْذَلِ الْعُمْرِ ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ الدُّنْيَا وَعَذَابِ الْقَبْرِ .

"Ewe Mwenyezi Mungu najilinda kwako

kutokana na ubakhili, na najilinda kwako kutokana na uwoga, na najilinda kwako kutokana na kurudishwa kwenye umri duni, na najilinda kwako kutokana na fitna ya dunia na adhabu ya kaburi.”

(٦١) اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْجَنَّـةَ وأَعُـوْذُ بِـكَ مِنَ النَّارِ .

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nakuomba pepo, na najilinda kwako kutokana na moto.”

(٦٢) اللَّهُمَّ بِعِلْمِكَ الْغَيْـبِ وَقُدْرَتِـكَ عَلَـى الْخَلْقِ أَحْيِنِـي مَـا عَلِمْـتَ الْحَيَـاةَ خَـيْراً لِـي وَتَوَفَّنِي إِذَا عَلِمْتَ الْوَفَاةَ خَـيْراً لِـي ، اللَّهُـمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ خَشْيَتَكَ فِي الْغَيْبِ وَالشَّـهَادَةِ ،

وَأَسْأَلُكَ كَلِمَةَ الْحَقِّ فِي الرِّضَا وَالْغَضَبِ ، وَأَسْأَلُكَ الْقَصْدَ فِي الْغِنَى وَالْفَقْرِ ، وَأَسْأَلُكَ نَعِيماً لاَ يَنْفَدُ ، وَأَسْأَلُكَ قُرَّةَ عَيْنٍ لاَ تَنْقَطِعُ ، وَأَسْأَلُكَ الرِّضَا بَعْدَ الْقَضَاءِ ، وَأَسْأَلُكَ بَرْدَ الْعَيْشِ بَعْدَ الْمَوْتِ ، وَأَسْأَلُكَ لَذَّةَ النَّظَرِ إِلَى وَجْهِكَ وَالشَّوْقَ إِلَى لِقَائِكَ فِي غَيْرِ ضَرَّاءَ مُضِرَّةٍ وَلاَ فِتْنَةٍ مُضِلَّةٍ ، اللَّهُمَّ زَيِّنَّا بِزِينَةِ الْإِيمَانِ وَاجْعَلْنَا هُدَاةً مُهْتَدِينَ .

“Ewe Mwenyezi Mungu, kwa ujuzi wako wa mambo yalio fichikana, na uwezo wako wa kuumba, niweke hai iwapo uhai ni bora kwangu, na nifishe iwapo kufa ni bora kwangu, Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nakuomba khofu yako kwa siri na dhahiri, na

ninakuomba neno la haki wakati nimefurahi na wakati nimekasirika, na ninakuomba matumizi ya wastani wakati wa utajiri na wakati wa umaskini, na ninakuomba neema isiyokwisha, na ninakuomba kituliza jicho (moyo) kisicho katika, na ninakuomba kuridhia baada yakuwa umesha nipangia, na nina kuomba maisha ya utulivu, baada ya kufa, na nina kuomba ladha yakukutizama uso wako, na shauku yakukutana nawe, pasina madhara yanayodhuru, wala fitna yenye kupoteza, Ewe Mwenyezi Mungu, tupambe kwa kipambo cha imani, na tujaalie tuwe waongozi wenye kuongoka."

(٦٣) اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ يَا اللَّهُ بِأَنَّكَ الْوَاحِدُ الْأَحَدُ الصَّمَدُ الَّذِى لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ وَلَمْ

يَكُنْ لَهُ كُفُواً أَحَدٌ أَنْ تَغْفِرَ لِي ذُنُوبِي إِنَّكَ أَنْتَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ .

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nakuomba, Ewe Mwenyezi Mungu kwa vile Wewe ni Mmoja ulie pekee, Mwenye kutegemewa kwa haja zote, ambae hakuzaa wala hakuzaliwa, na wala hakuna mfano wake na kitu chochote, nakuomba unisamehe makosa yangu, hakika Wewe ni Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu."

(٦٤) اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ بِأَنَّ لَكَ الْحَمْدُ لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ وَحْدَكَ لاَ شَرِيكَ لَكَ ، الْمَنَّانُ ، يَا بَدِيعَ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضِ يَاذَا الْجَلاَلِ وَالإِكْرَامِ ، يَاحَيُّ يَاقَيُّومُ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْجَنَّةَ

وأَعُوْذُ بِكَ مِنَ النَّارِ .

"Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi nakuomba, kwa vilesifa njema zote ni zako, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe, hali yakuwa pekeyako, huna mshirika, mwingi wa kuneemesha, Ewe mtangulizi (muumbaji) wa mbingu na ardhi, (bila kuwa na mfano kabla), Ewe mwenye utukufu na ukarimu, Ewe alie hai mwenye kusimama kwa dhati yako, hakika mimi nakuomba Pepo, na najilinda kwako kutokana na moto."

(٦٥) اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ بِأَنِّي أَشْهَدُ أَنَّكَ أَنْتَ اللَّهُ لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ الأَحَدُ الصَّمَدُ الَّذِى لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُواً أَحَدٌ .

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi

nakuomba kwa vile ninakiri kwa hakika kwamba Wewe ni Mwenyezi Mungu, hapana apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe, hali ya kuwa pekee, mwenye kutegemewa kwa haja zote, ambae hakuzaa wala hakuzaliwa, na wala hakuna mfano wake na kitu chochote."

**25. Nyiradi baada ya kutoa Salamu (kumaliza Swala).**

(٦٦) أَسْتَغْفِرُ اللَّهَ ، أَسْتَغْفِرُ اللَّهَ ، أَسْتَغْفِرُ اللَّهَ .

"Namuomba msamaha Mwenyezi Mungu." (mara tatu)

اللَّهُمَّ أَنْتَ السَّلامُ ، ومِنْكَ السَّلامُ ، تَبارَكْتَ يَاذَا الْجَلاَلِ وَالإِكْرَامِ .

“Ewe Mwenyezi Mungu Wewe ndie Amani, na kwako ndiko kutokako amani, Umetukuka Ewe mwenye utukufu, na Ukarimu.”

(٦٧) لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيكَ لَهُ ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ، اللَّهُمَّ لاَ مَانِعَ لِمَا أَعْطَيْتَ ، وَلاَ مُعْطِيَ لِمَا مَنَعْتَ ، وَلاَ يَنْفَعُ ذَا الْجَدِّ مِنْكَ الجَدُّ .

“Hapana apasae kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu hali ya kuwa peke yake hana mshirika, niwake Ufalme, na nizake sifa njema, na yeye ni muweza wa kila kitu, Ewe Mwenyezi Mungu, hapana anaeweza kukizuia ulichokitoa, na wala kutoa ulichokizuia, na wala

haumnufaishi mwenye utajiri, kwani kwako Wewe ndio utajiri."

(٦٨) لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ لاَشَرِيكَ لَهُ ، لَـهُ الْمُلْكُ ، وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُـوَ عَلَـى كُـلِّ شَـيْءٍ قَدِيرٌ. لاَ حَوْلَ وَلاَ قُوَّةَ إِلاَّ  بِاللَّـهِ ، لاَإِلَـهَ إِلاَّ اللَّـهُ ، وَلاَ نَعْبُـدُ إِلاَّ إِيَّـاهُ ، لَـهُ النِّعْمَـةُ وَلَـهُ الْفَضْلُ وَلَـهُ الثَّنَـاءُ الْحَسَـنُ ، لاَ إِلَـهَ إِلاَّ اللَّـهُ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ .

"Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu hali ya kuwa peke yake hana mshirika wake, ni wake Ufalme, na nizake sifa njema, na Yeye juu ya kila kitu ni Mueza, hapana uwezo wala nguvu ila vyote vinatokana na Mwenyezi Mungu, hapana mola apasae

kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu, wala hatumuabudu ila Yeye, nizake neema, na niwake ubora, na nizake sifa nzuri zote, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu, hali ya kumtakasia dini yake, ijapokuwa wanachukia makafiri"

(٦٩) سُبْحَانَ اللَّهِ ( ثلاثًا وثلاثين )

"Ametakasika Mwenyezi Mungu" (mara thelathini na tatu )

الْحَمْدُ لِلَّهِ ( ثلاثًا وثلاثين )

"Sifa njema zote niza Mwenyezi Mungu" (mara thelathini na tatu )

اللَّهُ أَكْبَرُ ( ثلاثًا وثلاثين )

"Mwenyezi Mungu ni Mkubwa" ( mara thelathini na tatu )

لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ لاَشَرِيكَ لَهُ ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ .

"Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mwenyezi Mungu, hali ya kuwa peke yake hana mshirika wake, ni wake Ufalme, na ni zake sifa njema, na Yeye ni Mueza wa kila kitu."

*Kisha atasoma:* Suratul-Ikhlas, *na* Suratul-Falaq *na* Suratu-Nnas, *yaani* -

(٧٠) ﴿ قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ... ﴾

﴿ قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ... ﴾

*na*

﴿ قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ... ﴾

*na*

*kila baada ya swala mara moja, na*

*baada ya swala ya Magharibi na ya Alfajiri atazisoma hizo mara tatu tatu.*

*Pia ni katika Sunnah kusoma* Aayatul-Kursiy *baada ya kila swala. Nayo ni:*

(٧١) ﴿ اللَّهُ لاَ إِلَهَ إِلاَّ هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ لاَ تَأْخُذُهُ سِنَةٌ وَلاَ نَوْمٌ... ﴾ [ Suratul-Baqarah:255 ]

(٧٢) لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ لاَشَرِيكَ لَهُ ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ يُحْيِي وَيُمِيتُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ .

"Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki, ila Mwenyezi Mungu, hali yakuwa peke yake, hana mshirika wake, ni wake Ufalme, na nizake sifa njema, anahayaisha, anafisha, na yeye nimuweza kwa kila kitu." (Mara kumi baada ya Swala ya Alfajiri na ya Magharibi)

(٧٣) اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ عِلْماً نَافِعاً ، وَرِزْقاً طَيِّباً ، وَعَمَلاً مُتَقَبَّلاً .

"Ewe Mwenyezi Mungu nakuomba elimu yenye kunufaisha, na riziki iliyo nzuri, na ibada yenye kukubaliwa." (Baada ya kutoa Salamu ya Swala ya Alfajiri).

**26. Dua ya Swalatul-Istikhara (Swala ya kutaka muelekezo au kukata shauri katika jambo).**

*(74) Amesema Jaabir bin Abdillah* ﵁*: 'Alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu* ﷺ *akitufundisha Swala ya Istikhara kama vile anavyotufunza sura ya Qur'an, anasema* ﷺ*: 'Akikusudia mmoja wenu kufanya jambo aswali rakaa mbili zisizo za faradhi, kisha aseme:*

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْتَخِيرُكَ بِعِلْمِكَ ، وَأَسْتَقْدِرُكَ

بِقُدْرَتِـكَ ، وَأَسْـأَلُكَ مِـنْ فَضْلِـكَ الْعَظِيـمِ ، فَإِنَّكَ تَقْدِرُ وَلاَ أَقْدِرُ ، وَتَعْلَــمُ ، وَلاَ أَعْلَـمُ ، وَأَنْتَ عَلاَّمُ الْغُيُوبِ ، اللَّهُمَّ إِنْ كُنْــتَ تَعْلَـمُ أَنَّ هَذَا الأَمْرَ – ( وَيُسَمَّى حَاجَتَهُ ) – خَيْرٌ لِـي فِي دِينِي وَمَعَاشِــي وَعَاقِبَـةِ أَمْـرِي [عَاجِلِـهِ وَآجِلِهِ ] فَاقْدِرْهُ لِي وَيَسِّرْهُ لِــي ثُـمَّ بَـارِكْ لِي فِيهِ ، وَإِنْ كُنْتَ تَعْلَمُ أَنَّ هَذَا الأَمْـرَ شَـرٌّ لِي فِي دِينِي وَمَعَاشِي وَعَاقِبَةِ أَمْرِي [عَاجِلِهِ وَآجِلِـهِ ] فَاصْرِفْـهُ عَنِّـي وَاصْرِفْنِـي عَنْــهُ وَاقْدِرْ لِيَ الْخَيْرَ حَيْثُ كَانَ ثُمَّ أَرْضِنِي بِهِ .

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nakutaka muelekezo kwa ujuzi wako, na

nakuomba uniwezeshe kwa uwezo wako, na nakuomba fadhila zako kubwa, hakika Wewe unaweza, nami siwezi nawe unajua nami sijui, nawe nimjuzi wa yale yalio fichikana. Ewe Mwenyezi Mungu, iwapo jambo hili kutokana na ujuzi wako - *(atalitaja jambo lake)* - linakheri na mimi katika dini yangu na maisha yangu na mwisho wa jambo langu (karibu au mbali) basi nakuomba uniwezeshe ni lipate, na unifanyie wepesi, kisha unibariki, na iwapo unajua kwamba jambo hili ni shari kwangu katika dini yangu na maisha yangu na mwisho wa jambo langu ( karibu au mbali) basi liepushe na mimi nami niepushe nalo, na nipangie jambo jengine lenye kheri nami popote lilipo, kisha niridhishe kwalo."

*Na hajuti mwenye kumtaka muelekeo Mwenyezi Mungu, na akawashauri waja*

*waumini, na akajidhatiti katika jambo lake.*

*Amesema Mwenyezi Mungu (S.W) kumwambia Mtume wake ﷺ:*

﴿ وَشَاوِرْهُمْ فِي الْأَمْرِ فَإِذَا عَزَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ ﴾

"Na ushauriane nao katika mambo, na ukiazimia kufanya jambo, basi tegemea kwa Mwenyezi Mungu." ( Suratu Al-Imran: 159)

**27. Nyiradi za asubuhi na jioni.**

*Imepokewa kutoka kwa Anas رضي الله عنه amesema, amesema Mtume ﷺ: 'Kukaa pamoja na watu wanaomtaja Mwenyezi Mungu (S.W) kuanzia Swala ya Al-Fajiri mpaka kuchomoza jua kunapendeza zaidi kwangu mimi kuliko kuacha huru watu*

*wanne miongoni mwa wana wa Ismail, na kukaa na watu wanaomtaja Mwenyezi Mungu (S.W) kuanzia baada ya Swala ya Alasiri mpaka kuchwa jua kunapendeza zaidi kwangu mimi kuliko kuwaacha huru watu wanne.'*

(٧٥) ﴿ اللَّهُ لاَ إِلَهَ إِلاَّ هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ لاَ تَأْخُذُهُ سِنَةٌ وَلاَ نَوْمٌ... ﴾ [ Suratul-Baqarah:255 ]

*Mwenye kuisoma* **(Ayatul-Kursiy)** *pindi anapoamka atalindwa kutokana na majini mpaka jioni, na atakaeisoma jioni atalindwa nayo mpaka asubuhi.*

(٧٦) ﴿ قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ... ﴾

﴿ قُلْ أَعُوْذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ... ﴾

*na*

﴿ قُــلْ أَعُــوْذُ بِــرَبِّ النَّـــاسِ ... ﴾

*na*

(Mara tatu tatu)

*Mwenye kuzisoma (sura hizi) mara tatu asubuhi na jioni zinamtosheleza na kila kitu.*

(٧٧) أَصْبَحْنَا وَأَصْبَحَ الْمُلْكُ لِلَّـهِ وَالْحَمْـدُ لِلَّهِ ، لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيكَ لَهُ ، لَـهُ الْمُلْـكُ وَلَـهُ الْحَمْـدُ وَهُـوَ عَلَـى كُـلِّ شَـيْءٍ قَدِيرٌ ، رَبِّ أَسْأَلُكَ خَيْرَ مَا فِي هَذَا الْيَوْمِ ، وَخَيْرَ مَا بَعْدَهُ ، وَأَعُوْذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَـا فِـي هَذَا الْيَوْمِ وشَرِّ مَا بَعْدَهُ ، رَبِّ أَعُوْذُ بِكَ مِنَ الْكَسَلِ وَسُوءِ الْكِـبَرِ ، رَبِّ أَعُـوْذُ بِـكَ مِـنْ

عَذَابٍ فِي النَّارِ وَعَذَابٍ فِي الْقَبْرِ .

"Tumeingia wakati wa asubuhi na umekuwa Ufalme ni wa Mwenyezi Mungu, na sifa njema ni za Mwenyezi

"Mungu, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki, ila Mwenyezi Mungu, hali yakuwa peke yake, hana mshirika, niwake Ufalme, nanizake sifa njema, nayeye juu yakila kitu ni Mueza, Ewe mola; nakuomba kheri ya siku ya leo, na kheri ya baada ya siku hii, nanina jilinda kwako, kutokana na shari ya siku ya leo, na shari ya baada ya siku hii, Ewe Mola, najilinda kwako, kutokana na uvivu, na ubaya wa uzee ( uzee ubaya), Ewe Mola; najilinda kwako, kutokana na adhabu ya moto, na adhabu ya kaburi."

*Na akiingia jioni, atasema:*

أَمْسَيْنَا وَأَمْسَى الْمُلْكُ لِلَّهِ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ لاَ

شَرِيكَ لَهُ ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ، رَبِّ أَسْأَلُكَ خَيْرَ مَا فِي هَذِهِ اللَّيْلَةِ ، وَخَيْرَ مَا بَعْدَهَا ، وَأَعُوْذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا فِي هَذِهِ اللَّيْلَةِ وشَرِّ مَا بَعْدَهَا ، رَبِّ أَعُوْذُ بِكَ مِنَ الْكَسَلِ وَسُوءِ الْكِبَرِ ، رَبِّ أَعُوْذُ بِكَ مِنْ عَذَابٍ فِي النَّارِ وَعَذَابٍ فِي الْقَبْرِ.

(٧٨) اللَّهُمَّ بِكَ أَصْبَحْنَا وَبِكَ أَمْسَيْنَا ، وَبِكَ نَحْيَا ، وَبِكَ نَمُوتُ ، وَإِلَيْكَ النُّشُوْرُ .

"Ewe Mwenyezi Mungu kwa sababu yako tumeingia katika asubuhi, na kwa ajili yako tumeingia jioni, na kwa ajili yako ndio tumekuwa hai, na kwa ajili yako tutakufa, na kwako tutafufuliwa."

*Na ikifika jioni atasema:*

اللَّهُمَّ بِكَ أَمْسَيْنَا ، وبِكَ أَصْبَحْنَا ، وَبِكَ نَحْيَا وَبِكَ نَمُوتُ ، وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ

“Ewe Mwenyezi Mungu kwa ajili yako tumefika jioni, na kwa ajili yako tumefika asubuhi, na kwa ajili yako tukohai, na kwa ajili yako tutakufa, na nikwako tuu marejeo.”

(٧٩) اللَّهُمَّ أَنْتَ رَبِّي لاَ إِلَهَ إلاَّ أَنْتَ ، خَلَقْتَنِي وَأَنَا عَبْدُكَ ، وَأَنَا عَلَى عَهْدِكَ وَوَعْدِكَ مَا اسْتَطَعْتُ ، أَعُوْذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا صَنَعْتُ ، أَبُوءُ لَكَ بِنِعْمَتِكَ عَلَيَّ ، وَأَبُوءُ بِذَنْبِي فَاغْفِرْ لِي فَإِنَّهُ لاَيَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلاَّ أَنْتَ .

“Ewe Mwenyezi Mungu Wewe ni Mola wangu, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe, umeniumba mimi, na mimi ni mja wako, nami niko juu ya

ahadi yako, na agano lako, kiasi cha iwezo wangu, najilinda kwako, kutokana na shari ya nilicho kifanya, nakiri kwako kwa kunineemesha, nanakiri kwa madhambi yangu, basi nakuomba unisamehe kwani hasamehe madhambi ila Wewe."

kwa haki ila Wewe, umeniumba mimi, na mimi ni mja wako, nami nikojuu ya ahadi yako, na kiaga chako, kiasi cha uwezo wangu, najilinda kwako kutokana na shari ya nilichokifanya, narejea kwako kwa kunineemesha, na narejea kwa madhambi yangu, basi nakuomba unisamehe, kwani hasamehe madhambi ila Wewe."

(٨٠) اللَّهُمَّ إِنِّي أَصْبَحْتُ أُشْهِدُكَ ، وَأُشْهِدُ حَمَلَـةَ عَرْشِـكَ ، وَمَلائِكَتَـكَ ، وَجَمِيـعَ

خَلْقِكَ ، أَنَّكَ أَنْتَ اللّٰهُ لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ ،
وَحْدَكَ لاَشَرِيكَ لَكَ ، وأَنَّ مُحَمَّداً عَبْدُكَ
وَرَسُولُكَ . ( أربع مرات حين يصبح أو يمسي )

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nimefika asubuhi nakushuhudia na nina washuhudiza wabeba wa arshi yako, na malaika wako, na viumbe vyako vyote, kwamba Wewe ndiye Mwenyezi Mungu, hapana apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe,hali ya kuwa peke yako huna mshirika, na kwamba Muhammad ni mja wako, na ni mtume wako."

(Atasema hivi mara inne, asubuhi au jioni).

*...atakae yasema haya asubuhi au jioni mara inne, Mwenyezi Mungu (S.W) atamuepusha na moto.*

(٨١) اللَّهُمَّ مَا أَصْبَحَ بِي مِنْ نِعْمَةٍ ، أَوْ
بِأَحَدٍ مِنْ خَلْقِكَ ، فَمِنْكَ وَحْدَكَ لاَشَرِيكَ

لَكَ ، فَلَكَ الْحَمْدُ وَلَكَ الشُّكْرُ .

"Ewe Mwenyezi Mungu sikuamka na neema yoyote au kati ya kiumbe chako chochote, na neema ila inatoka kwako, hali ya kuwa pekeyako huna mshirika wako, ni zako sifa njema na nizako shukrani." ....*atakae yasema haya kila asubuhi basi atakuwa ametekeleza shukrani ya siku nzima, na atakae yasema jioni atakuwa ametekeleza shukrani ya usiku mzima.*

(٨٢) اللَّهُمَّ عَافِنِي فِي بَدَنِي ، اللَّهُمَّ عَافِنِي فِي سَمْعِي ، اللَّهُمَّ عَافِنِي فِي بَصَرِي ، لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ . (ثلاثًا)

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوْذُ بِكَ مِنَ الْكُفْرِ ، وَالْفَقْرِ ، وأَعُوْذُ بِكَ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ ، لاَ إِلَهَ إِلاَّ

أَنْتَ. ( ثلاثًا )

"Ewe Mwenyezi Mungu nipe afya ya mwili wangu, Ewe Mwenyezi Mungu nipe afya ya usikizi wangu, Ewe Mwenyezi Mungu nipe afya ya uwoni wangu, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe". ( mara tatu )

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi najilinda kwako kutokana na ukafiri, na ufakiri, na najilinda kwako kutokana na adhabu ya kaburi, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe."

( mara tatu )

(٨٣) حَسْبِيَ اللَّهُ لاَ إِلَهَ إِلاَّ هُوَ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَهُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ .

"Mwenyezi Mungu ananitosha, hapana

mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Yeye, kwake Yeye nimetegemea, na Yeye ni Mola wa arshi tukufu." (mara saba asubuhi na jioni)

(٨٤) اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْعَفْوَ وَالْعَافِيَةَ فِي الدُّنْيَا وَالأَخِرَةِ ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْعَفْوَ وَالْعَافِيَةَ فِي دِينِي ، وَدُنْيَايَ وَأَهْلِي ، وَمَالِي ، اللَّهُمَّ اسْتُرْ عَوْرَتِي ، وَآمِنْ رَوْعَاتِي ، اللَّهُمَّ احْفَظْنِي مِنْ بَيْنِ يَدَيَّ ، وَمِنْ خَلْفِي ، وَعَنْ يَمِينِي ، وَعَنْ شِمَالِي ، وَمِنْ فَوْقِي ، وَأَعُوذُ بِعَظَمَتِكَ أَنْ أُغْتَالَ مِنْ تَحْتِي .

"Ewe Mwenyezi Mungu nakuomba msamaha na afya duniani na akhera. Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi

nakuomba msamaha na afya katika dini yangu, na dunia yangu na jamaa zangu, na mali yangu, Ewe Mwenyezi Mungu nisitiri uchi wangu, na unitulize khofu yangu, Ewe Mwenyezi Mungu ni hifadhi mbele yangu, na nyuma yangu, na kulia kwangu, na kushoto kwangu, najuu yangu, na najilinda kwa utukufu wako kwakutekwa chini yangu."

(٨٥) اللَّهُمَّ عَالِمَ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضِ ، رَبَّ كُلِّ شَيْءٍ وَمَلِيكَهُ ، أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ ، أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ نَفْسِي ، وَمِنْ شَرِّ الشَّيْطَانِ وَشِرْكِهِ ، وَأَنْ أَقْتَرِفَ عَلَى نَفْسِي سُوءاً ، أَوْ أَجُرَّهُ إِلَى مُسْلِمٍ .

“Ewe Mwenyezi Mungu, Mjuzi wa yaliyojificha na yaliyowazi, Muumba wa mbingu na ardhi, Mola wa kila kitu, na Mfalme wake, nakiri kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe, najilinda kwako kutokana na shari ya nafsi yangu, na shari ya shetani na shirki yake, na kujichumia uovu kwa nafsi yangu au kumletea muislamu.”

(٨٦) بِسْمِ اللَّهِ الَّذِي لاَيَضُرُّ مَعَ اسْمِهِ شَيْءٌ فِي الأَرْضِ وَلاَ فِي السَّمَاءِ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ .

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, ambae hakidhuru kwa jina lake kitu chochote kile kilicho ardhini, wala mbinguni, nae ni Msikivu nani Mjuzi.”
(mara tatu).

(٨٧) رَضِيتُ بِاللَّهِ رباً ، وَبِالْإِسْلَامِ دِينـاً ، وَبِمُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَ سَلَّمٌ نَبياً .

"Nimeridhia kuwa Mwenyezi Mungu ndie Mola wangu, na uislamu ndio dini yangu, na Muhammad ﷺ kuwa ni Mtume wangu." (mara tatu)

(٨٨) يَـاحَيُّ يَـاقَيُّومُ بِرَحْمَتِـكَ أَسْـتَغِيثُ أَصْلِحْ لِي شَأْنِي كُلَّهُ وَلاَ تَكِلْنِي إِلَى نَفْسِـي طَرْفَةَ عَيْنٍ .

"Ewe Uliyehai, Uliyesimama kwa dhati yako, kwa rehema zako ninakuomba uniokoe, nitengenezee mambo yangu yote, wala usiniachie mambo yangu mwenyewe (pasina kunisaidia), hata kwa muda (mdogo kama muda) wa kupepesa jicho."

(٨٩) أَصْبَحْنَا وَأَصْبَحَ الْمُلْكُ لِلَّهِ رَبِّ العَالَمِينَ ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ خَيْرَ هَذَا الْيَوْمِ ، فَتْحَهُ ، وَنَصْرَهُ ، وَنُورَهُ وَبَرَكَتَهُ ، وَهُدَاهُ ، وأَعُوْذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا فِيهِ وَشَرِّ مَا بَعْدَهُ .

"Tumeingia asubuhi, na imefika asubuhi na Ufalme ni wa Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe vyote, Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nakuomba kheri ya siku hii ya leo, ufunguzi wake, na nusra yake, na nuru yake, na baraka yake, na uongofu wake, na najilinda kwako kutokana na shari ya kilicho ndani ya siku hii, na shari ya baada ya siku hii."

*Na ikiingia jioni atasema:*

أَمْسَيْنَا وَأَمْسَى الْمُلْكُ لِلَّهِ رَبِّ العَالَمِينَ ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ خَيْرَ

هَذِهِ اللَّيْلَةِ ، فَتْحَهَا ، وَنَصْرَهَا ، وَنُورَهَا وَبَرَكَتَهَا ، وَهُدَاهَا، وأَعُوْذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا فِيهَا وَشَرِّ مَا بَعْدَهَا.

(٩٠) أَصْبَحْنَا عَلَى فِطْرَةِ الإِسْلامِ ، وَعَلَى كَلِمَةِ الإِخْلاَصِ ، وَعَلَى دِينِ نَبِيِّنَا مُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمْ وَعَلَى مِلَّةِ أَبِينا إِبْرَاهِيمَ حَنِيفاً مُسْلِماً وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ .

"Tumeingia asubuhi na maumbile ya kiislamu, na neno la ikhlasi, na dini ya Mtume wetu Muhammad ﷺ na mila (dini) ya baba yetu Ibrahim iliyo sawa hali yakuwa muislamu wala hakuwa ni mwenye kumshirikisha Mwenyezi Mungu."

*Na ikiingia jioni atasema:*

أَمْسَيْنَا عَلَى فِطْرَةِ الإِسْلامِ ، وَعَلَى كَلِمَةِ الإِخْلاَصِ ، وَعَلَى دِينِ

نَبِيِّنَا مُحَمَّدٍ صَلَى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمْ وَعَلَى مِلَّـةِ أَبِينَـا إِبْرَاهِيـمَ حَنِيفـاً مُسْلِماً وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ .

(٩١) سُبْحَانَ اللَّهِ وبِحَمْدِهِ .

"Ametakasika Mwenyezi Mungu, na sifa njema zote nizake." (mara mia moja)

(٩٢) لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ ، وَحْدَهُ لاَشَرِيكَ لَـهُ ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلَـى كُـلِّ شَـيْءٍ قَدِيرٌ .

"Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mwenyezi Mungu, peke yake, hana mshirika wake, niwake Ufalme, na nizake sifa njema zote, na Yeye juu ya kila kitu ni Mueza."

(mara kumi, au mara moja ukisikia uvivu)

*Amesema Mtume ﷺ : 'Mwenye kusema inapoingia asubuhi:*

(٩٣) لا إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ ، وَحْدَهُ لاَشَرِيكَ لَهُ ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ .

"Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mwenyezi Mungu peke yake, hana mshirika wake, niwake Ufalme, na nizake sifa njema zote, na Yeye juu ya kila kitu ni Mueza."

*......kwa siku mara mia, basi yeye ana thawabu za kuwaacha huru watumwa kumi na ataandikiwa thawabu mia moja, na atafutiwa madhambi mia moja, na atakuwa na kinga ya shetani kwa siku hiyo yote hadi jioni, na hata kuwa mtu*

*yoyote mbora kumshinda, ila yule aliyefanya zaidi yake.*

(٩٤) سُبْحَانَ اللَّهِ وبِحَمْـدِهِ عَـدَدَ خَلْقِـهِ ، وَرِضَا نَفْسِهِ ، وَزِنَةَ عَرْشِهِ ، وَمِدَادَ كَلِمَاتِهِ.

"Ametakasika Mwenyezi Mungu, na sifa njema zote ni zake, kwa hisabu ya viumbe vyake, na radhi yake, na uzito wa arshi yake, na wino wa maneno yake." ( mara tatu kila asubuhi)

(٩٥) اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ عِلْماً نَافِعاً ، وَرِزْقاً طَيِّباً ، وَعَمَلاً مُتَقَبَّلاً .

"Ewe Mwenyezi Mungu nakuomba elimu yenye kunufaisha, na riziki iliyo nzuri, na ibada yenye kukubaliwa."

(٩٦) أَسْـتَغْفِرُ اللَّـهَ وَأَتُـوبُ إِلَيْـهِ .

“Namuomba msamaha Mwenyezi Mungu, na ninarejea Kwake.” (Mara mia kwa siku)

*Alikuwa Mtume ﷺ akisema asubuhi na jioni:*

(٩٧) أَعُوذُ بِكَلِمَاتِ اللَّهِ التَّامَّـاتِ مِـنْ شَـرِّ مَا خَلَقَ .(ثلاث إذا أمسى)

“Najilinda na maneno ya Mwenyezi Mungu yaliyotimia kutokana na shari aliyoiumba.”(mara tatu jioni)

*...mwenye kuisoma jioni mara tatu hatodhuriwa na mdudu wa sumu (kama nyoka au kitumbo-nge) usiku huo.*

(٩٨) اللَّهُمَّ صَلِّ وَسَلِّمْ عَلَـى نَبِيِّنَـا مُحَمَّـدٍ

.“Ewe Mwenyezi Mungu mfikishie rehema na amani Mtume wetu

Muhammad."

..... *'Mwenye kuniombea rehema asubuhi mara kumi, na jioni mara kumi, nitamuombea shifaa (msamaha) siku ya kiama.'*

**28. Nyiradi za kulala.**

*(99) Alikuwa Mtume ﷺ akienda kulala usiku anakusanya viganja vyake kisha akivipuliza na akivisomea Suratul-Ikhlas, na Suratul-Falaq, na Suratu-Nnas, kisha akipangusa kwa hivyo viganja vyake kiasi anachoweza katika mwili wake, akianza kichwani na usoni na mbele.*

*(Akifanya hivyo mara tatu).*

*(100) Mtume ﷺ amesema: 'Ukienda kulala soma* **Ayatul-Kursiy** *mpaka uimalize kwani Mwenyezi Mungu ataendelea kukuhifadhi, wala hakukaribii shetani mpaka asubuhi.'*

﴿اللَّهُ لاَ إِلَهَ إِلاَّ هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ لاَ تَأْخُذُهُ سِنَةٌ وَلاَ نَوْمٌ...﴾

[ Suratul-Baqarah:255 ]

*(101) Amesema Mtume*ﷺ*: 'Anaesoma aya mbili za mwisho wa Suratul-Baqarah usiku zinamtosheleza.'*

﴿ءَامَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنْزِلَ إِلَيْهِ مِنْ رَبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ ....﴾

*mpaka mwisho wa sura).* (Suratul - Baqarah: 285-286)

*(102) Mtume* ﷺ *pia amesema: 'Akiamka mmoja wenu kutoka usingizini kisha akarudi basi akikukute kitanda kwa shuka yake mara tatu, na amtaje Mwenyezi Mungu, kwani hajui kilicho kuja baada yake. Na akilala aseme:*

بِاسْمِكَ رَبِّي وَضَعْتُ جَنْبِي وَبِكَ أَرْفَعُهُ ، فَإِنْ أَمْسَكْتَ نَفْسِي فَارْحَمْهَا ، وَإِنْ أَرْسَلْتَهَا فَاحْفَظْهَا ، بِمَا تَحْفَظُ بِهِ عِبَادَكَ الصَّالِحِينَ .

"Kwa jina lako Mola wangu, nimeweka ubavu wangu na kwa ajili yako nitaunyanyua, na ukiizuia (ukiichukuwa) roho yangu, basi irehemu, na ukiirudisha basi ihifadhi, kwa kile unacho wahifadhi nacho waja wako wema."

(١٠٣) اللَّهُمَّ إِنَّكَ خَلَقْتَ نَفْسِي وَأَنْتَ تَوَفَّاهَا ، لَكَ مَمَاتُهَا وَمَحْيَاهَا ، إِنْ أَحْيَيْتَهَا فَاحْفَظْهَا ، وَإِنْ أَمَتَّهَا فَاغْفِرْ لَهَا. اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْعَافِيَةَ .

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika Wewe umeiumba nafsi yangu nawe utaiua, ni kwako uhai wa nafsi yangu na ufaji wake, ukiipa uhai basi ihifadhi, na ukiifisha (ukiiua) basi isamehe. Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nakuomba afya njema."

*Alikuwa Mtume ﷺ akitaka kulala, anaweka mkono wake wa kulia chini ya shavu lake, kisha anasema:*

(١٠٤) اللَّهُمَّ قِنِي عَذَابَكَ يَوْمَ تَبْعَثُ عِبَادَكَ.

"Ewe Mwenyezi Mungu nikinge mimi kwa adhabu yako siku utakayo wafufua waja wako."

(Mara tatu)

(١٠٥) بِاسْمِكَ اللَّهُمَّ أَمُوتُ وَأَحْيَا .

"Kwa jina lako Ewe Mwenyezi Mungu ninakufa na ninakuwa hai."

*(106) Mtume ﷺ amesema: 'Hivi niwafahamishe juu ya kitu ambacho ni bora zaidi kuliko mtumishi, wakati munapolala; msabihini Mwenyezi Mungu mara thelathini na tatu, kisha msifuni Mwenyezi Mungu mara thelathini na tatu, na kisha mkabirini mara thelathini na nne, kwani kufanya hivi ni bora kwenu kuliko mtumishi.'*

*(Yaani useme:*

سُبْحَانَ اللَّهِ

"Ametakasika Mwenyezi Mungu"
( mara thelathini na tatu )

وَالْحَمْدُ لِلَّهِ

"Sifa njema zote ni za Mwenyezi

Mungu."  ( mara thelathini na tatu )

اللَّهُ أَكْبَرُ

"Mwenyezi Mungu ni mkubwa."
( mara thelathini na nne )

(١٠٧) اللَّهُـمَّ رَبَّ السَّـمَوَاتِ السَّـبْعِ ، وَرَبَّ الْعَـرْشِ الْعَظِيـمِ ، رَبَّنَـا وَرَبَّ كُـلِّ شَيْءٍ ، فَالِقَ الْحَبِّ وَالنَّـوَى وَمُـنزِّلَ التَّـوْرَاةِ وَالإِنْجِيلِ ، وَالْفُرْقَانِ ، أَعُـوْذُ بِـكَ مِـنْ شَـرِّ كُلِّ شَيْءٍ أَنْتَ آخِـذٌ بِنَاصِيَتِـهِ. اللَّهُـمَّ أَنْـتَ الأَوَّلُ فَلَيْـسَ قَبْلَـكَ شَـيْءٌ ، وَأَنْـتَ الآخِـرُ فَلَيْـسَ بَعْـدَكَ شَـيْءٌ ، وَأَنْـتَ الظَّـاهِرُ فَلَيْـسَ فَوْقَكَ شَيْءٌ ، وَأَنْـتَ الْبَـاطِنُ فَلَيْـسَ دُونَـكَ

شَيْءٌ ، اِقْضِ عَنَّا الدَّيْنَ وَأَغْنِنَا مِنَ الْفَقْرِ .

"Ewe Mwenyezi Mungu, Mola wa mbingu saba, na Mola wa arshi tukufu, Mola wetu, na Mola wakila kitu, Mwenye kuichanua tembe ya mbegu na kokwa, na alie teremsha Taurat na Injiil,na Qur'ani, najikinga kwako, kutokana na shari ya kila kitu, Wewe ndie mwenye kukamata utosi wake, Ewe Mwenyezi Mungu, wewe ndie wa Mwanzo, hakuna kabla yako kitu, nawe ndie wa Mwisho, hakuna baada yako kitu, nawewe ndie uliewazi, hakuna juu yako kitu chochote, na Wewe ndie uliefichika, hakuna kilicho jificha chini yako, tulipie madeni yetu, na utuepushe na ufakiri."

(١٠٨) الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِى أَطْعَمَنَا وَسَقَانَا ، وَكَفَانَا ، وَآوَانَا ، فَكَمْ مِمَّنْ لاَ كَافِيَ لَهُ وَلاَ مُؤْوِيَ .

"Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye ametulisha na ametunywesha na akatutosheleza na akatuhifadhi, ni wangapi amb*ao* hawana wa kuwatosheleza wala wa kuwahifadhi."

(١٠٩) اللَّهُمَّ عَالِمَ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضِ ، رَبَّ كُلِّ شَيْءٍ وَمَلِيكَهُ ، أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ ، أَعُوْذُ بِكَ مِنْ شَرِّ نَفْسِي ، وَمِنْ شَرِّ الشَّيْطَانِ وَشِرْكِهِ ، وَأَنْ أَقْتَرِفَ عَلَى نَفْسِي سُوءاً ، أَوْ أَجُرَّهُ إِلَى مُسْلِمٍ .

"Ewe Mwenyezi Mungu Mjuzi wa yaliojificha na yaliowazi , Muumba wa mbingu na ardhi, Mola wa kila kitu na

Mfalme wake, nakiri kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe, najilinda kwako na shari ya nafsi yangu na shari ya shetani na shirki yake, na kujichumia uovu kwa nafsi yangu au kumletea muislamu."

*(110) Mtume ﷺ alikuwa halali mpaka asome* Suratu-Sajda *na* Suratul-Mulk.

*Ukitaka kulala tawadha udhu kama wa swala kisha lalia ubavu wako wa kulia kisha useme:*

(١١١) اللَّهُمَّ أَسْلَمْتُ نَفْسِي إِلَيْكَ ، وَفَوَّضْتُ أَمْرِي إِلَيْكَ ، وَوَجَّهْتُ وَجْهِي إِلَيْكَ ، وَأَلْجَأْتُ ظَهْرِي إِلَيْكَ ، رَغْبَةً وَرَهْبَةً إِلَيْكَ ، لاَ مَلْجَأَ وَلاَ مَنْجَا مِنْكَ إِلاَّ إِلَيْكَ ،

آمَنْتُ بِكِتَابِكَ الَّذِي أَنْزَلْتَ وَبِنَبِيِّكَ الَّذِي أَرْسَلْتَ .

"Ewe Mwenyezi Mungu nimeisalimisha nafsi yangu kwako, na nimekuachia mambo yangu Wewe, na nime uelekeza uso wangu kwako, na nimeutegemeza mgongo wangu kwako, kwa matarajio na kwa kukuogopa, hapana sehemu ya kukimbilia wala ya kujiokoa ila kwako, nimekiamini kitabu chako ulicho kiteremsha, na mtume wako uliyemtuma."

*Amesema Mtume ﷺ kwa mwenye kusema haya: 'Kisha ukifa utakuwa umekufa katika uislamu.'*

**29. Dua anapojigeuza usingizini usiku.**

(١١٢) لاَإِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ، رَبُّ

السَّـمَوَاتِ وَالأَرْضِ وَمَـا بَيْنَهُمَـا الْعَزِيـزُ الْغَفَّارُ.

"Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu, Mmoja, Alieshinda, Mola wa mbingu na ardhi na vilivyo kati yake, Aliyetukuka Mwingi wa Msamaha."

**30. Dua ya wasiwasi usingizini au kusikia uoga na mfazaiko.**

(١١٣) أَعُـوْذُ بِكَلِمَـاتِ اللَّـهِ التَّامَّـاتِ مِـنْ غَضَبِهِ وَعِقَابِهِ ، وَشَرِّ عِبَادِهِ ، وَمِـنْ هَمَـزَاتِ الشَّيَاطِينِ وَأَنْ يَحْضُرُونِ .

"Najilinda na maneno ya Mwenyezi Mungu yalio timia, kutokana na hasira zake, na adhabu yake, na shari ya waja

wake, na vioja vya mashetani na kuniijia kwao."

### 31. Anayoyafanya mwenye kuota ndoto njema au mbaya.

*Ndoto njema inatoka kwa Mwenyezi Mungu na ndoto mbaya inatoka kwa mashetani.*

*(114) Akiona mmoja wenu ndoto nzuri asimzungumzie ila yule anaempenda, na anaeona ndoto mbaya anatakiwa apulize kushotoni kwake mara tatu.*

*-Kisha atake (aombe) hifadhi, kwa Mwenyezi Mungu na alichokiona, na kwa shetani mara tatu.*

*- Kisha hatakiwi kumzungumzia mtu.*

*- Kisha asilalie ule upande au ubavu aliyootea, bali ageuke ubavu mwengine.*

(115) Atasimama kusali akitaka.

## 32. Dua ya Qunut ya Witri

(١١٦) اللَّهُمَّ اهْدِنِي فِيمَنْ هَدَيْتَ ، وَعَافِنِي فِيمَنْ عَافَيْتَ ، وَتَوَلَّنِي فِيمَنْ تَوَلَّيْتَ ، وَبَارِكْ لِي فِيمَا أَعْطَيْتَ ، وَقِنِي شَرَّ مَا قَضَيْتَ ، فَإِنَّكَ تَقْضِي وَلاَ يُقْضَى عَلَيْكَ ، إِنَّهُ لاَيَذِلُّ مَنْ وَالَيْتَ ، [ وَلاَ يَعِزُّ مَنْ عَادَيْتَ ]، تَبَارَكْتَ رَبَّنَا وَتَعَالَيْتَ .

”Ewe Mwenyezi Mungu, niongoze pamoja na uliowaongoza, na unipe afya njema, pamoja nauliowapa afya njema, na nifanye kuwa nimpenzi wako, pamoja na ulio wafanya wapenzi, na nibariki katika ulichonipa, na nikinge na shari ya ulilolihukumu, kwani Wewe unahukumu wala huhukumiwi, hakika hadhaliliki

uliemfanya mpenzi [wala hatukuki uliemfanya adui] Umetakasika Ewe Mola wetu na Umetukuka."

(١١٧) اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوْذُ بِرِضَاكَ مِنْ سَخَطِكَ ، وَبِمُعَافَاتِكَ مِنْ عُقُوبَتِكَ ، وَأَعُوْذُ بِكَ مِنْكَ ، لاَ أُحْصِي ثَنَاءً عَلَيْكَ ، أَنْتَ كَمَا أَثْنَيْتَ عَلَى نَفْسِكَ .

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi najilinda kwa radhi zako kutokana na hasira zako, na kwa msamaha wako kutokana na adhabu yako, na najilinda kwako kutokana na Wewe, mimi siwezi kuzidhibiti sifa zako, Wewe ni kama ulivyojisifu Mwenyewe."

(١١٨) اللَّهُمَّ إِيَّاكَ نَعْبُدُ ، وَلَكَ نُصَلِّي

وَنَسْجُدُ ، وَإِلَيْكَ نَسْعَى وَنَحْفِدُ ، نَرْجُوا رَحْمَتَكَ ، وَنَخْشَى عَذَابَكَ ، إِنَّ عَذَابَكَ بِالْكَافِرِينَ مُلْحَقٌ. اللَّهُمَّ إِنَّا نَسْتَعِينُكَ ، وَنَسْتَغْفِرُكَ ، وَنُثْنِي عَلَيْكَ الْخَيْرَ ، وَلاَ نَكْفُرُكَ ، وَنُؤْمِنُ بِكَ ، وَنَخْضَعُ لَكَ ، وَنَخْلَعُ مَنْ يَكْفُرُكَ .

"Ewe Mwenyezi Mungu, Wewe tu ndie tunaabudu, na kwako tunasali na tunasujudu, na kwako tunakimbilia na tunakutumikia, tunataraji rehema yako, na tunaogopa adhabu yako, kwani adhabu yako hakuna shaka kuwa makafiri itawafikia. Ewe Mwenyezi Mungu hakika sisi tunakutaka msaada, na tunakutaka msamaha, na tunakusifu kwa kheri, na

wala hatuku kufurishi, na tunakuamini Wewe, na tunakunyenyekea na tunamuepuka anaekukufuru."

**33. Dua baada ya Salamu katika Swala ya Witri.**

(١١٩) سُبْحَانَ الْمَلِكِ الْقُدُّوسِ

"Ametakasika Mwenyezi Mungu, Mfalme, Mtakatifu." (Mara tatu)

*Na mara ya tatu anaisoma kwa sauti kubwa na kwa kuivuta.*

رَبِّ الْمَلائِكَةِ وَالرُّوحِ .

"Ewe Mola wa malaika na wa jibril."

**34. Dua ukiwa na hamu na huzuni.**

(١٢٠) اللَّهُمَّ إِنِّي عَبْدُكَ ، ابْنُ عَبْدِكَ ، ابْنِ

أَمَتِكَ ، نَاصِيَتِي بِيَدِكَ ، مَاضٍ فِيَّ حُكْمُكَ ، عَدْلٌ فِيَّ قَضَاؤُكَ، أَسْأَلُكَ بِكُلِّ اسْمٍ هُوَ لَكَ ، سَمَّيْتَ بِهِ نَفْسَكَ ، أَوْ أَنْزَلْتَهُ فِي كِتَابِكَ ، أَوْ عَلَّمْتَهُ أَحَداً مِنْ خَلْقِكَ ، أَوِ اسْتَأْثَرْتَ بِهِ فِي عِلْمِ الْغَيْبِ عِنْدَكَ ، أَنْ تَجْعَلَ الْقُرْآنَ رَبِيعَ قَلْبِي ، وَنُورَ صَدْرِي ، وَجَلاءَ حُزْنِي ، وَذَهَابَ هَمِّي .

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ni mtumwa wako, mtoto wa mtumwa wako, mtoto wa kijakazi chako, utosi wangu uko mikononi mwako, yaliyopita kwangu yako katika hukumu yako, ni usawa kwangu kunihukumu kwako, nakuomba kwa kila jina ambalo ni Lako

ulilojiita kwalo Mwenyewe, au ulilolitleremsha katika kitabu chako, au ulilomfundisha yoyote yule kati ya viumbe vyako, au ulilolihifadhi Wewe mwenyewe (na kujihusisha kulijuwa) katika ilimu ilio fichika kwako, nakuomba uijaalie(uifanye) Qur'ani, kuwa ni raha na uchanuzi wa roho yangu, na nuru ya kifua changu, nautatuzi wa huzuni yangu, nasababu ya kuondoka majonzi yangu."

(١٢١) اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْهَمِّ وَالْحُزْنِ ، وَالْعَجْزِ وَالْكَسَلِ ، وَالْبُخْلِ وَالْجُبْنِ ، وَضَلَعِ الدَّيْنِ وَغَلَبَةِ الرِّجَالِ .

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi najilinda kwako kutokana na hamu na huzuni na kutoweza na uvivu na ubakhili

na uoga na uzito wa deni na kushindwa na watu."

**35. Dua ya kupatwa na janga au balaa.**

(١٢٢) لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ الْعَظِيمُ الْحَلِيمُ ، لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ رَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ ، لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَرَبُّ الأَرْضِ وَرَبُّ الْعَرْشِ الْكَرِيمِ .

"Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mwenyezi Mungu, aliye Mtukufu Mpole, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mwenyezi Mungu, Mola wa Arshi tukufu, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mwenyezi Mungu Mola wa mbingu na Mola wa ardhi, na Mola wa arshi tukufu."

(١٢٣) اللَّهُمَّ رَحْمَتَكَ أَرْجُو فَلاَ تَكِلْنِي إِلَى نَفْسِي طَرْفَةَ عَيْنٍ، وَأَصْلِحْ لِي شَأْنِي كُلَّهُ، لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ.

"Ewe Mwenyezi Mungu rehema zako nataraji, usinitegemeze kwenye nafsi yangu japo kwa muda wa upepesa jicho, na unitengenezee mambo yangu yote, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe."

(١٢٤) لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ.

"Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe, kutakasika ni Kwako, hakika mimi ni miongoni mwa waliodhulumu nafsi zao."

(١٢٥) اللَّهُ اللَّهُ رَبِّي لاَ أُشْرِكُ بِهِ شَيْئاً .

“Mwenyezi mungu, Mwenyezi Mungu, Mola wangu simushirikishe na kitu chochote kile.”

**36. Dua ya anaekutana na adui au mwenye kutawala.**

(١٢٦) اللَّهُـمَّ إِنَّـا نَجْعَلُـكَ فِـي نُحُورِهِـمْ وَنَعُوذُ بِكَ مِنْ شُرُورِهِمْ .

“Ewe Mwenyezi Mungu hakika sisi tunakufanya Wewe uwe katika vifua vyao, na tunajikinga kwako na shari zao.”

(١٢٧) اللَّهُـمَّ أَنْـتَ عَضُـدِي ، وَأَنْـتَ نَصِيرِي ، بِكَ أَجُولُ ، وَبِكَ أَصُـولُ ، وَبِـكَ أُقَاتِلُ .

"Ewe Mwenyezi Mungu Wewe ndie msaidizi wangu, nawe ndie mnusuru wangu, kwako ninazunguka, na kwako ninavamia, na kwako ninapigana."

(١٢٨) حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ .

"Mwenyezi Mungu anatutosheleza, naye ni mbora wa kutegemewa."

**37. Dua ya mwenye kuogopa dhulma ya mwenye kutawala.**

(١٢٩) اللَّهُـمَّ رَبَّ السَّـمواتِ السَّـبْعِ ، وَرَبَّ الْعَـرْشِ الْعَظِيْـمِ ، كُـنْ لِـي جَـاراً مِـنْ فُلاَنِ بْنِ فُلاَنٍ ، وَأَحْزَابِهِ مِنْ خَلاَئِقِـكَ ، أَنْ يَفْـرُطَ عَلَـيَّ أَحَـدٌ مِنْهُـمْ أَوْ يَطْغَـى ، عَـزَّ جَارُكَ ، وَجَلَّ ثَنَاؤُكَ ، وَلاَ إِلَـهَ إِلاَّ أَنْـتَ .

Ewe Mwenyezi Mungu, Mola wa mbingu saba, na Mola wa arshi tukufu, kuwa mlinzi wangu kutokana na fulani bin fulani, na vikosi vyake miongoni mwa viumbe vyako, kwakunisaliti mmoja miongoni mwao, au kunifanyia uadui, amehishimiwa mwenye umelinda, nazimetukuka sifa zako, na hapana mola apasae kuabudiwa kwa uhaki, ila Wewe."

(١٣٠) اللَّهُ أَكْبَرُ ، اللَّهُ أَعَزُّ مِنْ خَلْقِهِ جَمِيْعاً ، اللَّهُ أَعَزُّ مِمَّا أَخَافُ وَأَحْذَرُ ، أَعُوذُ بِاللَّهِ الَّذِي لاَإِلَهَ إِلاَّ هُوَ ، الْمُمْسِكِ السَّموَاتِ السَّبْعِ أَنْ يَقَعْنَ عَلَى الْأَرْضِ إِلاَّ بِإِذْنِهِ ، مِنْ شَرِّ عَبْدِكَ فُلاَنٍ ، وَجُنُودِهِ وَأَتْبَاعِهِ وَأَشْيَاعِهِ ، مِنَ الْجِنِّ وَالإِنْسِ ،

اللَّهُمَّ كُنْ لِي جَاراً مِنْ شَرِّهِمْ ، جَلَّ ثَنَاؤُكَ وَعَزَّ جَارُكَ ، وَتَبَارَكَ اسْمُكَ وَلاَ إِلَهَ غَيْرُكَ

(130) Mwenyezi Mungu ni mkubwa, Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu(cheo) kuliko viumbe vyake vyote, Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu, kuliko kila nikiogopacho nakujihadhari, najikinga na Mwenyezi Mungu, ambae hapana mola ila yeye tuu, ambae ameshikililia mbingu saba, ili zisi angukie ardhi, ila kwa idhini yake, kutokana na shari ya mja wako fulani, na majeshi yake, nawanae mfuata, na wafuasi wake, miongoni mwa majini na watu. Ewe Mwenyezi Mungu, kuwa mlinzi wangu kutokana nashari yao, zimetukuka sifa zako, na umehishimika

ulinzi wako, nalime takasika jina lako, na hapana apasae kuabudiwa kwa uhaki, asie kuwa Wewe.

**38. Kuomba dua dhidi ya adui.**

(١٣١) اللَّهُمَّ مُنْزِلَ الْكِتَابِ ، سَرِيعَ الْحِسَابِ ، اِهْزِمِ الأَحْزَابَ ، اللَّهُمَّ اهْزِمْهُمْ وَزَلْزِلْهُمْ .

"Ewe Mwenyezi Mungu, Mteremsha wa kitabu, Mwepesi wa kuwahisabu (waja wako), vishinde vikosi. Ewe Mwenyezi Mungu, washinde na watetemeshe."

**39. Dua ya anaewaogopa watu.**

(١٣٢) اللَّهُمَّ اكْفِنِيهِمْ بِمَا شِئْتَ .

"Ewe Mwenyezi Mungu, nitoshelezee kutokana na wao kwa unacho taka."

**40. Dua ya aliyepatwa na shaka katika imani yake.**

*(113) Atataka (aombe) hifadhi ya Mwenyezi Mungu.*
*-Aondowe kile kitu alicho kifanyia shaka.*

- *kisha aseme:-*

(١٣٤) آمَنْتُ بِاللّٰهِ وَرُسُلِهِ .

"Nimemuamini Mwenyezi Mungu na mitume yake."

*Kisha asome aya hii katika Qur'ani:-*

(١٣٥) ﴿ هُوَ الأَوَّلُ ، وَالآخِرُ ، وَالظَّاهِرُ وَالْبَاطِنُ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴾

"Yeye ndiye wa Mwanzo, na wa Mwisho, na aliye Wazi, na aliye Jificha, naye ni mjuzi wa kila kitu."

**41. Dua ya kulipa deni.**

(١٣٦) اللَّهُمَّ اكْفِنِي بِحَلاَلِكَ عَنْ حَرَامِكَ وَأَغْنِنِي بِفَضْلِكَ عَمَّنْ سِوَاكَ .

"Ewe Mwenyezi Mungu nitosheleze mimi na halali yako kutokana na haramu, na unitosheleze kwa fadhila zako nisiwahitaji wengine usio Wewe."

(١٣٧) اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوْذُ بِكَ مِنَ الْهَمِّ وَالْحُزْنِ ، وَالْعَجْزِ وَالْكَسَلِ ، وَالْبُخْلِ وَالْجُبْنِ ، وَضَلَعِ الدَّيْنِ وَغَلَبَةِ الرِّجَالِ .

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi najilinda kwako kutokana na hamu, na huzuni, na kutoweza, na uvivu, na ubakhili na uoga, na uzito wa deni, na kushindwa na watu."

**42. Dua ya aliyeingiwa na wasiwasi katika Swala yake au kisomo chake.**

(١٣٨) أَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ .

*"Najilinda na Mwenyezi Mungu, kutokana na shetani aliyelaaniwa."*

*..kisha utatema vijimate vichache, upande wa kushoto mara tatu.*

*Imepokewa kutoka kwa Uthman Ibn Al-Ass* ﷺ *amesema: 'Nilimwambia Mtume; Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu hakika shetani amenikalia kati yangu na kati ya swala yangu na kisomo changu, ananitatiza.' Akasema Mtume* ﷺ*: 'Huyo Ni shetani aitwae "Khanzab" ukimuhisi amekuijia, basi muombe hifadhi Mwenyezi Mungu nae, natema vijimate vichache kushotoni kwako, mara tatu.*

*....nika fanya hivyo Mwenyezi Mungu akaniondoshea."*

**43. Dua ya ambaelimekua gumu kwake jambo.**

(١٣٩) اللَّهُمَّ لاَسَهْلَ إِلاَّ مَا جَعَلْتَهُ سَهْلاً

وَأَنْتَ تَجْعَلُ الْحَزْنَ إِذَا شِئْتَ سَهْلاً .

"Ewe Mwenyezi Mungu hakuna jepesi ila ulilolifanya jepesi, nawe unalifanya gumu jepesi ukitaka."

**44. Analosema aliyefanya dhambi.**

*(140) 'Hakuna mja yoyote yule anaefanya dhambi kisha akatawadha vizuri na akaswali rakaa mbili, kisha akamtaka Mwenyezi Mungu msamaha ila atasamehewa.'*

**45. Dua ya kumfukuza shetani na wasiwasi wake.**

*Mambo yafuatayo yanatakiwa kufuatwa*

*pindi anapotolewa shetani:*

*(141) Kumuomba Mwenyezi Mungu akuhifadhi nae.*

*(142) Kumuadhinia.*

*(143) Kusoma nyiradi zilizopokewa kutoka kwa Mtume ﷺ, na kusoma Qur'ani.*

**46. Dua anayoisoma mtu akitokewa na jambo asiloliridhia au akishindwa kufanya jambo.**

*Amesema Mtume ﷺ: 'Mumini mwenye nguvu ni bora na anapendeza zaidi kwa Mwenyezi Mungu kuliko mumini dhaifu, na wote wana kheri, fanya pupa kwa kile kitakacho kunufaisha na taka msaada kwa Mwenyezi Mungu wala usichoke, na kikikupata kitu chochote kibaya basi usiseme* **lau** *kama ningefanya kadha na kadha yasingenitokea haya, lakini sema:*

(١٤٤) قَدَّرَ اللَّهُ وَمَا شَاءَ فَعَلَ

*"Amepanga Mwenyezi Mungu na analolitaka anafanya."*

*.....hakika neno la* **lau** *linafungua matendo ya shetani.*

*Hakika Mwenyezi Mungu analaumu mwenye kukata tamaa, lakini usivunjike moyo, na ukishindwa na jambo kabisa sema:*

حَسْبِيَ اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ

"Mwenyezi Mungu ananitosheleza, naye ni Mbora wa kutegemewa."

**47. Pongezi ya kupata mtoto na jawabu yake.**

(١٤٥) بَارَكَ اللَّهُ لَكَ فِي الْمَوْهُوبِ لَكَ ،

وَشَكَرْتَ الْوَاهِبَ ، وَبَلَغَ أَشُدَّهُ ، وَرُزِقْتَ بِرَّهُ.

"Mwenyezi Mungu akubariki katika ulicho pewa na umshukuru aliyekupa, na afike kuwa mkubwa, na uruzukiwe wema wake."

*Na aliyepongezwa atamuombea aliyempongeza kwa kumwambia:*

بَارَكَ اللَّهُ لَكَ وَبَارَكَ عَلَيْكَ ، وَجَزَاكَ اللَّهُ خَيْراً ، وَرَزَقَكَ اللَّهُ مِثْلَهُ ، وَأَجْزَلَ ثَوَابَكَ .

"Mwenyezi Mungu akubariki na ateremshe baraka juu yako, na Mwenyezi Mungu akujazi kheri, na Mwenyezi Mungu akuruzuku mfano wake, na afanye nyingi thawabu zako."

**48.Dua inayo kingwa nayo watoto.**

*Imepokelewa na Ibn Abbas amesema:*

*alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu akiwakinga wajukuu wake (Hassan na Hussein), akisema:*

(١٤٦) أُعِيذُكُمَا بِكَلِمَاتِ اللَّهِ التَّامَّةِ مِنْ كُلِّ شَيْطَانٍ وَهَامَّةٍ ، وَمِنْ كُلِّ عَيْنٍ لاَمَّةٍ .

"Nawakinga kwa maneno ya Mwenyezi Mungu yaliyotimia, awakinge kutokana na kila shetani, na uvamizi, na kila jicho lenye kudhuru."

**49. Dua ya kumtembelea mgonjwa.**

*Alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ anapoingia kumzuru mgonjwa akimwambia:*

(١٤٧) لاَبَأْسَ طَهُورٌ إِنْ شَاءَ اللَّهُ .

"Hakuna neno, (ugonjwa) ni kusafishwa (na madhambi), anapopenda Mwenyezi Mungu."

*Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: 'Hapana mja yoyote muislamu anaemtembelea mgonjwa ambae wakati wake wa kufa bado haujafika na akamuombea mara saba:*

(١٤٨) أَسْأَلُ اللَّهَ الْعَظِيمَ رَبَّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ أَنْ يَشْفِيَكَ .

"Namuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mola wa Arshi tukufu (akuponyeshe)."

*Isipokuwa Mwenyezi Mungu humponyesha mgonjwa huyo.*

**50. Fadhila za kumtembelea mgonjwa.**

(149) Imepokewa na Ali bin Abi Twalib amesema, nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akisema: "Mtu anapomtembelea ndugu yake muislamu

mgonjwa, basi hutembelea katika bustani ya peponi mpaka atakapo keti, na anapo keti hufunikwa, na rehma, ikiwa ni asubuhi, wanamtakia rehma malaika sabini elfu mpaka jioni, na ikiwa ni jioni wanamtakia rehema malaika sabini elfu mpaka asubuhi" .

### 51. Dua anayoomba mgonjwa aliyekata tamaa na kupona.

(١٥٠) اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي وَارْحَمْنِي وَأَلْحِقْنِي بِالرَّفِيقِ الأَعْلَى .

"Ewe Mwenyezi Mungu, nisamehe mimi, na uni rehemu, na unikutanishe na waja walio katika daraja za juu."

*(151) Imepokewa kutoka kwa Aisha (R.A) amesema: 'Mtume ﷺ wakati anakufa alikuwa akiingiza mikono yake*

*ndani ya maji kisha akipangusa kwayo uso wake na akisema;*

لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ إِنَّ لِلْمَوْتِ لَسَكَرَاتٍ.

"Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki, ila ni Mwenyezi Mungu ,hakika kifo kina uchungu."

(١٥٢) لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ ، لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ ، لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ لاَشَرِيكَ لَهُ ، لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ ، لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ ولاَحَوْلَ ولاَقُوَّةَ إِلاَّ بِاللَّهِ .

"Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni Mkubwa, Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila ni

Mwenyezi Mungu peke yake, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mwenyezi Mungu, mpeke hana mshirika wake, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mwenyezi Mungu, ni wake Ufalme, na sifa njema zote ni zake, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mwenyezi Mungu, na hapana uwezo wala nguvu isipokuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu."

**52. Kumlakinia anaetokwa na roho.**

*(153) Amesema Mtume ﷺ : 'Mwenye kuwa neno lake la mwisho;*

لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ.

"Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Mwenyezi Mungu."

...... *ataingia peponi.'*

## 53. Dua ya aliyepatwa na msiba.

(١٥٤) إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ اللَّهُمَّ أْجُرْنِي فِي مُصِيبَتِي وَأَخْلِفْ لِي خَيْراً مِنْهَا .

"Sisi ni wa Mwenyezi Mungu nasi kwake tutarejea, Ewe Mwenyezi Mungu nilipe kwa msiba wangu, na unipe badili yake bora kuliko huo."

## 54. Dua ya kumfunga macho maiti.

(١٥٥) اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِفُلاَنٍ ( باسمه ) وَارْفَعْ دَرَجَتَهُ فِي الْمَهْدِيِّينَ ، وَاخْلُفْهُ فِي عَقِبِهِ فِي الْغَابِرِينَ ، وَاغْفِرْ لَنَا وَلَهُ يَارَبَّ الْعَالَمِينَ ، وَافْسَحْ لَهُ فِي قَبْرِهِ وَنَوِّرْ لَهُ فِيهِ .

"Ewe Mwenyezi Mungu msamehe-(jina la

maiti) – na ipandishe daraja yake katika walioongoka, na weka badili yake kwa aliyoyawacha nyuma, na utusamehe sisi na yeye Ewe Mola wa viumbe vyote, na umkunjulie yeye katika kaburi lake na umtilie mwangaza ndani yake."

**55. Dua ya kumuombea maiti wakati anaposwaliwa.**

(١٥٦) اللَّهُمَّ اغْفِرْ لَهُ وَارْحَمْهُ ، وَعَافِهِ ، وَاعْفُ عَنْهُ ، وَأَكْرِمْ نُزُلَهُ ، وَوَسِّعْ مُدْخَلَهُ ، وَاغْسِلْهُ بِالْمَاءِ وَالثَّلْجِ وَالْبَرَدِ ، وَنَقِّهِ مِنَ الْخَطَايَا كَمَا نَقَّيْتَ الثَّوْبَ الأَبْيَضَ مِنَ الدَّنَسِ ، وَأَبْدِلْهُ دَاراً خَيْراً مِنْ دَارِهِ ، وَأَهْلاً خَيْراً مِنْ أَهْلِهِ ، وَزَوْجاً خَيْراً مِنْ زَوْجِهِ ،

وَأَدْخِلْهُ الْجَنَّةَ ، وَأَعِذْهُ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ

[وَعَذَابِ النَّارِ] .

"Ewe Mwenyezi Mungu msamehe na umrehemu, na umuafu, na msamehe, na mtukuze kushuka kwake (kaburini), na upanue kuingia kwake, na muoshe na maji, na kwa theluji, na barafu, na mtakase namakosa, kama unavyo takasa nguo nyeupe kutokana na uchafu, na mbadilishie nyumba bora kuliko nyumba yake, na jamaa bora kuliko jamaa zake, na mke bora kuliko mke wake, na muingize peponi na mkinge na adhabu ya kaburi [na adhabu ya moto]."

(١٥٧) اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِحَيِّنَا ، وَمَيِّتِنَا ،

وَشَاهِدِنَا ، وَغَائِبِنَا ، وَصَغِيرِنَا وَكَبِيرِنَا ،

وَذَكَرِنَا وَأُنْثَانَا. اللَّهُــمَّ مَـنْ أَحْيَيْتَـهُ مِنَّـا فَأَحْيِـهِ عَلَـى الإِسْـلامِ ، وَمَـنْ تَوَفَّيْتَـهُ مِنَّـا فَتَوَفَّـهُ عَلَـى الْإِيمَـانِ ، اللَّهُـمَّ لاَ تَحْرِمْنَـا أَجْـرَهُ وَلاَ تُضِلَّنَـا بَعْدَهُ.

"Ewe mwenyezi Mungu msamehe aliyehai katika sisi na aliye kufa, na aliyopo na asiyekuwepo, na mdogo kati yetu na mkubwa, na mwanamume kati yetu na mwanamke. Ewe Mwenyezi Mungu unaemueka hai kati yetu basi mweke katika uislamu, na uliyemfisha basi mfishe juu ya imani. Ewe Mwenyezi mweke katika uislam, na unayemfisha usitupoteze baada yake."

(١٥٨) اللَّهُـمَّ إِنَّ فُـلاَنَ بْـنَ فُـلاَنٍ فِـي ذِمَّتِكَ ، وَحَبْلِ جِوَارِكَ ، فَقِهِ مِنْ فِتْنَـةِ الْقَبْرِ

وَعَذَابِ النَّارِ، وَأَنْتَ أَهْـلُ الْوَفَـاءِ وَالْحَـقِّ .
فَاغْفِرْ لَهُ وَارْحَمْهُ إِنَّكَ أَنْتَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ .

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika *fulani bin fulani* yuko katika dhima yako, na kamba ya ujirani wako basi mkinge na fitina ya kaburi na adhabu ya moto nawe ndiwe mstahiki wa utekelezaji na ukweli, basi msamehe na umrehemu hakika Wewe ni mwingi wa kusamehe, mwingi wa kurehemu."

(١٥٩) اللَّهُمَّ عَبْدُكَ وَابْنُ أَمَتِكَ احْتَاجَ إِلَى رَحْمَتِكَ ، وَأَنْتَ غَنِيٌّ عَنْ عَذَابِهِ ، إِنْ كَانَ مُحْسِناً فَزِدْ فِي حَسَنَاتِهِ ، وَإِنْ كَانَ مُسِيئاً فَتَجَاوَزْ عَنْهُ.

"Ewe Mwenyezi Mungu, mja wako na

mtoto wa kijakazi chako, nimuhitaji wa rehema yako, nawe huhitaji na kumuadhibu, kwa hivyo akiwa ni mwema mzidishie katika mema yake, na akiwa ni muovu msamehe madhambi yake."

**56. Dua ya maiti ya mtoto mchanga wakati wa kumswalia.**

(١٦٠) اللَّهُمَّ أَعِذْهُ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ .

"Ewe Mwenyezi Mungu mlinde na adhabu ya kaburi."

اللَّهُمَّ اجْعَلْهُ فَرَطاً وَذُخْراً لِوَالِدَيْهِ ، وَشَفِيعاً مُجَاباً. اللَّهُمَّ ثَقِّلْ بِهِ مَوَازِينَهُمَا وَأَعْظِمْ بِهِ أُجُورَهُمَا ، وَأَلْحِقْهُ بِصَالِحِ الْمُؤْمِنِينَ ، وَاجْعَلْهُ فِي كَفَالَةِ إِبْرَاهِيمَ ، وَقِهِ بِرَحْمَتِكَ

عَذَابَ الْجَحِيمِ ، وَأَبْدِلْهُ دَاراً خَيْراً مِـنْ دَارِهِ وَأَهْـلاً خَـيْراً مِـنْ أَهْلِـهِ ، اللَّهُـمَّ اغْفِـرْ لِأَسْلاَفِنَا ، وَأَفْرَاطِنَا ، وَمَنْ سَبَقَنَا بِالْإِيْمَانِ.

"Ewe Mwenyezi Mungu mjaalie kuwa nikitangulizi na akiba kwa wazazi wake na nikiombezi chenye kukubaliwa dua yake. Ewe Mwenyezi Mungu kwa ajili yake zifanye nzito mizani za wazazi wake na yafanye mengi malipo yao, namkutanishe na wema wa waumini, na mjaalie awe katika dhamana ya Ibrahim na umuepushe kwa rehema yako na adhabu ya moto, na mbadilishie nyumba bora kuliko nyumba yake, na jamaa bora kuliko jamaa zake, Ewe Mwenyezi Mungu wasamehe waliotangulia, na waliopita, na waliotutangulia katika Uislamu."

*Alikuwa Al-Hassan ﷺ anamsomea mtoto mdogo Suratul-Fatiha kisha akisema:*

(١٦١) اللَّهُـمَّ اجْعَلْـهُ لَنَـا فَرَطـاً ، وَسَـلَفاً ، وَأَجْراً .

"Ewe Mwenyezi Mungu, mfanye kwetu sisi ni kitangulizi cha malipo, na dhamana, namalipo."

**57. Dua ya kumtaazi (kumhani) aliyefiliwa.**

(١٦٢) إِنَّ لِلَّهِ مَا أَخَذَ ، وَلَهُ مَا أَعْطَى وَكُلُّ شَـيْءٍ عِنْـدَهُ بِـأَجَلٍ مُسَـمًّى... فَلْتَصْـبِرْ وَلْتَحْتَسِبْ .

"Kwa hakika nicha Mwenyezi Mungu alicho kichukua, na nichake alicho kitoa,

na kila kitu kwake kina muda maalumu, .... *(kisha Mtume ﷺ akamwambia),* basi vumilia na taka malipo kwa Mwenyezi Mungu."

*na akisema:*

أَعْظَمَ اللَّهُ أَجْرَكَ وَأَحْسَنَ عَزَاءَكَ وَغَفَرَ لِمَيِّتِكَ

"Ayafanye mengi Mwenyezi Mungu malipo yako, na akufanye kuzuri kutaaziwa (kuhaniwa) kwako na amsamehe maiti wako."

*.....basi ni bora.*

**58. Dua ya kumuingiza maiti ndani ya kaburi.**

(١٦٣) بِسْمِ اللَّهِ وعَلَى سُنَّةِ رَسُولِ اللَّهِ .

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu, na kwa mwenendo wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ.”

**59. Dua baada ya kumzika maiti.**

(١٦٤) اللَّهُمَّ اغْفِرْ لَهُ اللَّهُمَّ ثَبِّتْهُ . “Ewe Mwenyezi Mungu msamehe, Ewe Mwenyezi Mungu mfanye awethabiti.”

*Mtume (SAW) alikua akimaliza kuzika anasimama mbele ya kaburi na kisha anasema: ‘Muombeeni msamaha kwa Mwenyezi Mungu ndugu yenu na muombeeni kuthibitishwa kwani hivi sasa anaulizwa.’*

**60. Dua ya kuzuru makaburi.**

(١٦٥) السَّلامُ عَلَيْكُمْ أَهْلَ الدِّيَارِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُسْلِمِينَ ، وَ إِنَّا إِنْ شَاءَ اللَّهُ

بِكُمْ لاَحِقُونَ [وَيَرْحَمُ اللَّهُ الْمُسْتَقْدِمِينَ مِنَّـا وَالْمُسْتَأْخِرِينَ] أَسْأَلُ اللَّهَ لَنَا وَلَكُمُ الْعَافِيَةَ.

Amani ishuke juu yenu watu wa nyumba za waumini na waislamu, nasi apendapo Mwenyezi Mungu, tuta kutana nanyi, tuna muomba Mwenyezi Mungu atusamehe, sisi na nyinyi." [Na Mwenyezi Mungu, awarehemu, wa mwanzo, na wa mwisho] namuomba Mwenyezi Mungu, atupe sisi nanyi afya njema.

### 61. Dua ya upepo mkali.

(١٦٦) اللَّهُـمَّ إِنِّـي أَسْـأَلُكَ خَيْرَهَـا وأَعُـوْذُ بِكَ مِنْ شَرِّهَا .

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nakuomba kheri ya upepo huu, na

najikinga kwako na shari yake."

(١٦٧) اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ خَيْرَهَا ، وَخَيْرَ مَا فِيهَا ، وَخَيْرَ مَا أُرْسِلَتْ بِهِ وأَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّهَا ، وَشَرِّ مَا فِيهَا وَشَرِّ مَا أُرْسِلَتْ بِهِ .

"Ewe Mwenyezi Mungu nakuomba kheri yake na kheri ya kilicho ndani yake, na kheri ya uliyoituma ndani yake, na najikinga kwako kutokana na shari yake, na shari iliyoko ndani yake, na shari ilyotumwa nao."

**62. Dua ya radi.**

*Alikuwa Abdallah bin Zubeir ﷺ akisikia radi basi huacha mazungumzo, badala yake husema:*

(١٦٨) سُبْحَانَ الَّذِي يُسَبِّحُ الرَّعْدُ بِحَمْدِهِ

وَالْمَلائِكَةُ مِنْ خِيفَتِهِ .

"Ametakasika yule ambae radi zinamtakasa kwa sifa zake, na malaika pia kwa kumuogopa."

**63. Dua ya kuomba mvua.**

(١٦٩) اللَّهُمَّ أَسْقِنَا غَيْثاً مُغِيثاً مَرِيئاً مَرِيعاً ، نَافِعاً غَيْرَ ضَارٍّ ، عَاجِلاً غَيْرَ آجِلٍ .

"Ewe Mwenyezi Mungu tunyesheleze mvua yenye kuokoa, nyingi, yenye kustawisha, yenye manufaa isiyo dhuru, ya haraka isiyochelewa."

(١٧٠) اللَّهُمَّ أَغِثْنَا ، اللَّهُمَّ أَغِثْنَا ، اللَّهُمَّ أَغِثْنَا.

"Ewe Mwenyezi Mungu, tuokowe kwa

kututeremshia nvua, ewe Mwnyezi Mungu tuokowe kwa kututeremshia nvua, ewe Mwenyezi Mungu, tuokowe kwa kuteremshia nvua."

(١٧١) اللَّهُمَّ اسْقِ عِبَادَكَ ، وَبَهَائِمَكَ ، وَانْشُرْ رَحْمَتَكَ ، وَأَحْيِ بَلَدَكَ الْمَيِّتَ .

"Ewe Mwenyezi Mungu wanyesheleze waja wako, na wanyama wako, na eneza rehema zako, na fufua nchi yako iliyokufa."

**64. Dua ya mvua inaponyesha.**

(١٧٢) اللَّهُمَّ صَيِّباً نَافِعاً .

"Ewe Mwenyezi Mungu ijaalie yenye kumiminika yenye kunufaisha.'

**65. Dua baada ya mvua.**

(١٧٣) مُطِرْنَا بِفَضْلِ اللَّهِ وَرَحْمَتِهِ .

"Tumenyeshelezwa kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na rehema zake."

**66. Dua ya kutaka mvua iondoke (wakati itakapoleta madhara).**

(١٧٤) اللَّهُمَّ حَوَالَيْنَا وَلاَ عَلَيْنَا ، اللَّهُمَّ عَلَى الآكَامِ وَالظِّرَابِ ، وَبُطُونِ الأَوْدِيَةِ ، وَمَنَابِتِ الشَّجَرِ .

"Ewe Mwenyezi Mungu inyesheleze kwetu wala isiwe yenye kutuangamiza, Ewe Mwenyezi Mungu inyesheleze kwenye vichaka na milima, na mabonde, na kwenye mizizi ya miti."

**67 Dua ya kuona mwezi unaponaama (unapo andaama)**

(١٧٥) اللَّهُ أَكْبَرُ ، اللَّهُمَّ أَهِلَّهُ عَلَيْنَا بِـالْأَمْنِ وَالْإِيمَانِ ، وَالسَّلَامَةِ وَالْإِسْلَامِ ، وَالتَّوْفِيقِ لِمَا تُحِبُّ رَبَّنَا وَتَرْضَى ، رَبُّنَا وَرَبُّكَ اللَّهُ .

"Mwenyezi Mungu ni Mkubwa, Ewe Mwenyezi Mungu uanzishe kwetu kwa amani, na imani na usalama na uislamu, na taufiq ya kile unachokipenda Mola wetu na kukiridhia, Mola wetu na Mola wako ni Mwenyezi Mungu."

**68. Dua ya wakati wa kufungua saumu.**

(١٧٦) ذَهَـبَ الظَّمَـأُ ، وَابْتَلَّـتِ الْعُـرُوقُ ، وَثَبَتَ الْأَجْرُ إِنْ شَاءَ اللَّهُ .

"Kiu kimeondoka, na mishipa imelainika, na yamethibiti malipo Mwenyezi Mungu akipenda."

*Imepokewa kutoka kwa Abdillahi bin Amr bin Al Ass ﷺ, amesema: 'Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: 'Aliyefunga wakati wa kufuturu kwake, ana dua isiorudishwa.'*

(١٧٧) اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ بِرَحْمَتِكَ الَّتِي وَسِعَتْ كُلَّ شَيْءٍ أَنْ تَغْفِرَ لِي .

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nakuomba kwa rehema zako ambazo zimeenea kila kitu, unisamahe" .

**69. Dua kabla ya kula.**

*(178) "Atakapo kula mmoja wenu chakula basi aseme:*

بِسْمِ اللَّهِ .

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu."

*na akisahau mwanzo wake, basi aseme:*

بِسْمِ اللَّهِ فِي أَوَّلِهِ وَآخِرِهِ

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwanzo wake na mwisho wake."

*(179) Yoyote ambae Mwenyezi Mungu amemruzuku chakula aseme:*

اللَّهُمَّ بَارِكْ لَنَا فِيهِ وَأَطْعِمْنَا خَيْراً مِنْهُ

"Ewe Mwenyezi Mungu tubariki katika chakula hichi na tulishe bora kuliko hichi."

*na yoyote ambae ameruzukiwa maziwa basi aseme:*

اللَّهُمَّ بَارِكْ لَنَا فِيهِ وَزِدْنَا مِنْهُ

"Ewe Mwenyezi Mungu tubarikie kinywaji hichi na utuzidishie."

**70. Dua ya baada ya kula.**

(١٨٠) الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَطْعَمَنِي هَذَا ، وَرَزَقَنِيهِ ، مِنْ غَيْرِ حَوْلٍ مِنِّي وَلاَ قُوَّةٍ .

"Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu ambae amenilisha mimi chakula hichi na akaniruzuku pasina uwezo wangu wala nguvu zangu."

(١٨١) الْحَمْدُ لِلَّهِ حَمْداً كَثِيراً طَيِّباً مُبَارَكاً فِيهِ ، غَيْرَ [مَكْفِيٍّ وَلاَ ] مُوَدَّعٍ ، وَلاَ مُسْتَغْنًى عَنْهُ رَبُّنَا .

"Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, sifa nyingi, nzuri, zenye baraka ndani yake, zisizo toshelezwa, wala kuagwa wala kutoshwa nazo mtu, Ewe Mola wetu."

**71. Dua ya mgeni kwa aliyemkaribisha chakula.**

(١٨٢) اللَّهُمَّ بَارِكْ لَهُمْ فِيمَا رَزَقْتَهُمْ ، وَاغْفِرْ لَهُمْ وَارْحَمْهُمْ .

"Ewe Mwenyezi Mungu wabariki katika ulicho waruzuku na uwasamehe na uwarehemu."

**72. Dua ya kumuombea aliyekupa kinywaji au anaetaka kukupa.**

(١٨٣) اللَّهُمَّ أَطْعِمْ مَنْ أَطْعَمَنِي وَاسْقِ مَنْ سَقَانِي .

"Ewe Mwenyezi Mungu mlishe aliyenilisha, na mnyweshe aliyeninywesha."

**73. Dua ya kumuombea uliye futuru kwake.**

(١٨٤) أَفْطَرَ عِنْدَكُمُ الصَّائِمُونَ ، وَأَكَلَ طَعَامَكُمُ الأَبْرَارُ ، وَصَلَّتْ عَلَيْكُمُ الْمَلاَئِكَةُ.

"Wafuturu kwenu waliofunga, na wale chakula chenu watu wema, na wawaombee rehema malaika."

**74. Dua ya aliealikwa chakula lakini akawa amefunga.**

*(185) 'Akialikwa mmoja wenu aitike mwito, akiwa amefunga basi awaombee dua, na kama hakufunga basi ale.'*

**75. Anachosema aliyetukanwa hali ya kuwa amefunga.**

(١٨٦) إِنِّي صَائِمٌ ، إِنِّي صَائِمٌ .

“Hakika mimi nimefunga, hakika mimi nimefunga.”

**76. Dua ya kuomba unapoona matunda yanachipua kwenye miti.**

(١٨٧) اللَّهُمَّ بَارِكْ لَنَا فِي ثَمَرِنَا ، وَبَارِكْ لَنَا فِي مَدِينَتِنَا وَبَارِكْ لَنَا فِي صَاعِنَا ، وَبَارِكْ لَنَا فِي مُدِّنَا .

“Ewe Mwenyezi Mungu tubarikie matunda yetu, na tubarikie mji wetu, na tubarikie pishi (Swaa’) yetu, na tubarikie kibaba (Mudd) chetu.”

*(Swaa’ moja ni sawa na Mudd nne, na Mudd moja ni kipimo cha viganja vya mikono mara nne).*

**77. Dua ya kupiga chafya (kuchemua).**

*(188) ‘Akichemua mmoja wenu aseme:*

الْحَمْدُ لِلَّهِ

"Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu."

*Mwenzake amwambie:*

يَرْحَمُكَ اللَّهُ

"Mwenyezi Mungu akurehemu."

*Kisha naye amjibu:*

يَهْدِيكُمُ اللَّهُ وَيُصْلِحُ بَالَكُمْ

"Akuongoze Mwenyezi Mungu, na akutengenezee mambo yako."

**78. Anachoambiwa kafiri anapopiga chafya (chemua).**

(١٨٩) يَهْدِيكُمُ اللَّهُ وَيُصْلِحُ بَالَكُمْ .

"Mwenyezi Mungu akuongoze na

akurekebishie mambo yako."

**79. Dua ya kumuombea aliyeowa.**

(١٩٠) بَارَكَ اللَّهُ لَكَ ، وَبَارَكَ عَلَيْكَ ، وَجَمَعَ بَيْنَكُمَا فِي خَيْرٍ .

"Mwenyezi Mungu akubariki, na abariki juu yako, na awajumuishe katika kheri."

**80. Dua anayoomba bwana harusi, au aliyenunuwa chombo cha kupanda (kama mnyama au gari).**

(١٩١) اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ خَيْرَهَا وَخَيْرَ مَا جَبَلْتَهَا عَلَيْهِ ، وأَعُوْذُ بِكَ مِنْ شَرِّهَا وَشَرِّ مَا جَبَلْتَهَا عَلَيْهِ .

"Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi nakuomba kheri ya (mke) huyu, na kheri

ya maumbile uliyo muumba nayo, na najilinda kwako na shari yake, na shari ya maumbile ulio muumba nayo."

*Na akinunua mnyama atamshika kichwa chake na kisha atasoma dua hii.*

**81. Dua kabla ya kujimai.**

(١٩٢) بِسْمِ اللَّهِ ، اللَّهُمَّ جَنِّبْنَا الشَّيْطَانَ ، وَجَنِّبِ الشَّيْطَانَ مَا رَزَقْتَنَا .

"Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Ewe Mwenyezi Mungu tuepushe na shetani, na muepushe shetani na ulicho turuzuku."

**82. Dua ya wakati mtu amekasirika.**

(١٩٣) أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ .

"Najilinda kwa Mwenyezi Mungu

kutokana na shetani aliyeepushwa na kuwekwa mbali na rehema za Mwenyezi Mungu."

**83. Dua anayoomba mwenye kumuona kilema.**

(١٩٤) الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي عَافَانِي مِمَّا ابْتَلاَكَ بِهِ وَفَضَّلَنِي عَلَى كَثِيرٍ مِمَّنْ خَلَقَ تَفْضِيلاً .

"Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye ameniepusha na kile alichokupa mtihani, na akanifanya mimi kuwa bora kuliko wengi miongoni mwa aliowaumba."

**84. Utajo unaosomwa katika kikao.**

*(195) Imepokewa kutoka kwa Ibn Omar amesema: 'Alikuwa akihisabiwa Mtume* ﷺ *kusoma kwake dua hii katika kikao*

*kimoja ikifika idadi ya mara mia kabla haja simama.'*

رَبِّ اغْفِرْ لِي وَتُبْ عَلَيَّ إِنَّكَ أَنْـتَ التَّـوَّابُ الْغَفُورُ .

"Mwenyezi Mungu nisamehe, na nikubalie toba yangu, hakika Wewe ni mwingi wa kukubali toba, mwingi wa kusamehe."

**85. Kafara ya kikao.**

(١٩٦) سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وبِحَمْـدِكَ ، أَشْـهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ ، أَسْتَغْفِرُكَ وَأَتُـوْبُ إِلَيْـكَ

"Kutakasika ni kwako Ewe Mwenyezi Mungu, na sifa njema zote ni zako, nakiri kwamba hakuna mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe,

nakuomba msamaha na ninarejea kwako."

*Imepokewa kutoka kwa Aisha (R.A) amesema: 'Hajapatapo kukaa Mtume ﷺ kikao, wala kusoma Qur'ani, wala kuswali ila atamaliza na dua hii.' Amesema Aisha (R.A) nikamuuliza; 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu nakuona hukai kikao chochote wala husomi Qur'ani wala huswali swala yoyote ile ila unaimalizia kwa kusoma maneno haya, kwanini hasa? Akasema; Ndio anaisema kheri amalize kwa kheri, na anaesema shari yanakuwa maneno haya nikafara kwake."*

سُبْحَانَكَ وَبِحَمْدِكَ لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ أَسْتَغْفِرُكَ

وَ أَتُوْبُ إِلَيْكَ.

"Kutakasika ni kwako, na sifa njema zote

ni zako, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe, nakuomba msamaha, na ninarejea kwako."

**86. Kumuombea dua anaekuombea msamaha kwa Mwenyezi Mungu.**

*Imepokewa kutoka kwa Abdillahi bin Sarjis ﷺ amesema; 'Nilimjia Mtume (S.A..W) nikala katika chakula chake, kisha nikamwambia:*

غَفَرَ اللَّهُ لَكَ يَا رَسُولَ اللَّهِ.

"Mwenyezi Mungu akusamehe Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu."

*Akaniambia,*

وَ لَكَ. (١٩٧)

"Nawe akusamehe."

**87. Dua ya kumuombea aliyekufanyia wema.**

(١٩٨) جَزَاكَ اللَّهُ خَيْراً .

"Mwenyezi Mungu akulipe wema."

**88. Dua ya kujilinda na Dajjal.**

*(199) 'Yoyote anaehifadhi kwa moyo aya kumi za mwanzo wa* Suratul-Kahf *atakuwa na kinga ya kujiepusha na Dajjal.*

*Pia ni katika Sunnah kujilinda na Mwenyezi Mungu kutokana na fitna ya Dajjal baada ya tashahhud ya mwisho katika kila swala.*

**89. Dua ya kumuombea anaekwambia anakupenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.**

(٢٠٠) أَحَبَّكَ الَّذِي أَحْبَبْتَنِي لَهُ .

"Akupende ambae umenipenda mimi kwa ajili yake."

**90. Dua ya kumuombea aliyekusaidia kwa mali.**

(٢٠١) بَارَكَ اللَّهُ لَكَ فِي أَهْلِكَ وَمَالِكَ .

"Mwenyezi Mungu akubariki katika familia yako na mali yako."

**91. Dua unapolipa deni.**

(٢٠٢) بَارَكَ اللَّهُ لَكَ فِـي أَهْلِـكَ وَمَـالِكَ ، إِنَّمَا جَزَاءُ السَّلَفِ الْحَمْدُ وَالأَدَاءُ .

"Mwenyezi Mungu akubariki katika familia yako na mali yako, hakika malipo ya deni ni kushukuru na kulipa."

**92. Dua ya kuogopa kuingia katika ushirikina.**

(٢٠٣) اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ أَنْ أُشْرِكَ بِكَ وَأَنَا أَعْلَمُ ، وأَسْتَغْفِرُكَ لِمَا لاَ أَعْلَمُ .

"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi najilinda kwako kutokana na kukushirikisha hali ya kuwa najua, na ninakutaka msamaha na nisilolijua."

**93. Dua kwa aliyesema Mwenyezi Mungu akubariki.**

(٢٠٤) وَفِيْكَ بَارَكَ اللَّهُ.

"Na wewe Mwenyezi Mungu akubariki."

**94. Dua ya kuchukia ndege mbaya.**

(٢٠٥) اللَّهُمَّ لاَ طَيْرَ إِلاَّ طَيْرُكَ ، وَلاَ خَيْرَ إِلاَّ خَيْرُكَ ، وَلاَ إِلَهَ غَيْرُكَ .

"Ewe Mwenyezi Mungu hapana ndege

mbaya ila ndege wako, na hapana kheri ila kheri yako, na hapana apasae kuabudiwa kwa haki asie kuwa Wewe."

**95.Dua ya kupanda mnyama au chombo chochote cha kusafiria.**

(٢٠٦) بِسْمِ اللَّهِ ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ، ﴿ سُبْحَانَ الَّذِي سَخَّرَ لَنَا هَذَا وَمَا كُنَّا لَهُ مُقْرِنِينَ . وَإِنَّا إِلَى رَبِّنَا لَمُنْقَلِبُونَ ﴾ الْحَمْدُ لِلَّهِ ، الْحَمْدُ لِلَّهِ ، الْحَمْدُ لِلَّهِ ، اللَّهُ أَكْبَرُ ، اللَّهُ أَكْبَرُ ، اللَّهُ أَكْبَرُ ، سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي فَاغْفِرْ لِي ، فَإِنَّهُ لاَيَغْفِرُ الذُّنوبَ إِلاَّ أَنْتَ .

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu, na sifa

njema zote ni za Mwenyezi Mungu, ametakasika ambaye ametudhalilishia sisi hiki (chombo au huyu mnyama) na hatukuwa sisi kwacho ni wenye uwezo, nasi kwa Mola wetu tutarejeshwa. Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, sifa njema ni za Mwenyezi Mungu; Mwenyezi Mungu ni Mkubwa, Mwenyezi Mungu ni Mkubwa, Mwenyezi Mungu ni Mkubwa; Kutakasika ni Kwako Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi nimeidhulumu nafsi yangu basi nisamehe, kwani hakuna mwenye kusamehe madhambi ila Wewe."

**96. Dua ya safari.**

(٢٠٧) اللَّـهُ أَكْـبَرُ ، اللَّـهُ أَكْـبَرُ ، اللَّـهُ أَكْبَرُ ، ﴿سُبْحَانَ الَّـذِي سَخَّرَ لَنَا هَـذَا وَمَا

كُنَّا لَهُ مُقْرِنِينَ . وَإِنَّا إِلَى رَبِّنَا لَمُنْقَلِبُونَ ﴾
اللَّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ فِي سَفَرِنَا هَذَا الْبِرَّ وَالتَّقْوَى ، وَمِنَ الْعَمَلِ مَا تَرْضَى ، اللَّهُمَّ هَوِّنْ عَلَيْنَا سَفَرَنَا هَذَا وَاطْوِ عَنَّا بُعْدَهُ ، اللَّهُمَّ أَنْتَ الصَّاحِبُ فِي السَّفَرِ ، وَالْخَلِيفَةُ فِي الْأَهْلِ ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ وَعْثَاءِ السَّفَرِ ، وَكَآبَةِ الْمَنْظَرِ وَسُوءِ الْمُنْقَلَبِ فِي الْمَالِ وَالْأَهْلِ .

"Mwenyezi Mungu ni Mkubwa, Mwenyezi Mungu ni Mkubwa, Mwenyezi Mungu ni Mkubwa; ametakasika ambaye ametudhalilishia sisi hiki (chombo au huyu mnyama), na

hatukuwa sisi kwacho ni wenye uwezo, na sisi kwa Mola wetu tutarejeshwa. Ewe Mwenyezi Mungu hakika sisi tunakuomba katika safari yetu hii wema na ucha Mungu, na katika matendo unayoyaridhia, Ewe Mwenyezi Mungu ifanye nyepesi safari yetu hii, na ufupishe umbali wake, Ewe Mwenyezi Mungu, Wewe ndie Mwenzangu katika safari, na Mchungaji wa familia yangu, Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi najilinda kwako kutokana na ugumu wa safari, na ubaya wa mtizamo, na uovu wa kubadilikiwa katika mali na familia."

*Wakati wa kurudi safari atayasema haya yalioko juu na kisha atazidisha*:

آيِبُونَ تَائِبُونَ عَابِدُونَ لِرَبِّنَا حَامِدُونَ

"Tunarudi, hali ya kuwa tunatubia, tunaabudu, na Mola wetu tunamsifu."

**97. Dua ya kuingia mjini au kijijini.**

(٢٠٨) اللَّهُـمَّ رَبَّ السَّـمَوَاتِ السَّبْعِ وَمَـا أَظْلَلْنَ ، وَرَبَّ الْأَرَاضِينَ السَّبْعِ وَمَـا أَقْلَلْـنَ ، وَرَبَّ الشَّيَاطِينِ وَمَا أَضْلَلْـنَ ، وَرَبَّ الرِّيَـاحِ وَمَا ذَرَيْنَ. أَسْأَلُكَ خَيْرَ هَـذِهِ الْقَرْيَـةِ وَخَـيْرَ أَهْلِهَـا ، وَخَـيْرَ مَـا فِيهَـا ، وأَعُـوْذُ بِـكَ مِـنْ شَرِّهَا ، وشَرِّ أَهْلِهَا ، وشَرِّ مَا فِيهَا .

"Ewe Mwenyezi Mungu, Mola wa mbingu saba na kila ambacho hizo mbingu zimekipa kivuli, na Mola wa ardhi saba na kila ambacho zimebeba, na Mola wa mashetani na walicho kipoteza, na Mola wa upepo na ulicho kibeba, nakuomba kheri ya kijiji hichi, na kheri ya watu wake, na kheri ya

vilivyo ndani yake, najilinda kwako na shari ya kijiji hichi, na shari ya watu wake, na shari iliyomo ndani yake."

**98. Dua ya kuingia sokoni.**

(٢٠٩) لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ لاَشَرِيكَ لَهُ ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ ، يُحْيِي وَيُمِيتُ وَهُوَ حَيٌّ لاَ يَمُوتُ بِيَدِهِ الْخَيْرُ ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ .

"Hakuna mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu hali ya kuwa peke yake, hana mshirika, ni wake Ufalme, na ni zake sifa njema, anahuisha na anafisha, nae ni hai asiye kufa, kheri iko mikononi mwake, na Yeye juu ya kila kitu ni Mueza."

**99. Dua wakati mnyama alieupanda akileta tabu (au chombo cha safari).**

(٢١٠) بِسْمِ اللَّهِ .

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu.”

**100. Dua ya anaesafiri kuwaombea wakaazi.**

(٢١١) أَسْتَوْدِعُكُمُ اللَّهَ الَّذِي لاَ تَضِيعُ وَدَائِعُهُ .

“Nawaacha katika amana ya Mwenyezi Mungu ambaye hakupotei amana kwake.”

**101. Dua ya wakaazi wanayo muombea anae safiri.**

(٢١٢) أَسْتَوْدِعُ اللَّهَ دِينَكَ ، وَأَمَانَتَكَ ، وَخَوَاتِيمَ عَمَلِكَ .

"Naweka amana kwa Mwenyezi Mungu dini yako na uaminifu wako na mwisho wa matendo yako."

(٢١٣) زَوَّدَكَ اللَّهُ التَّقْوَى ، وَغَفَرَ ذَنْبَكَ ،
وَيَسَّرَ لَكَ الْخَيْرَ حَيْثُ مَا كُنْتَ .

"Mwenyezi Mungu akuzidishie ucha Mungu, na akusamehe madhambi yako, na akufanyie wepesi katika kheri popote ulipo."

### 102. Kumkumbuka Mwenyezi Mungu wakati wakupanda mlima na wakati wa kushuka.

*(214) Imepokelewa kutoka kwa Jaabir amesema: "Tulikuwa tukipandamlima tuna sema:*

اللَّهُ أَكْبَرُ

"Mwenyezi Mungu ni Mkubwa."

*Na tukishuka tunasema:*

سُبْحَانَ اللَّهِ

"Ametakasika Mwenyezi Mungu."

**103. Dua ya msafiri unapoingia usiku.**

(٢١٥) سَمِعَ سَامِعٌ بِحَمْدِ اللَّهِ ، وَحُسْنِ بَلاَئِهِ عَلَيْنَا ، رَبَّنَا صَاحِبْنَا ، وَأَفْضِلْ عَلَيْنَا عَائِذاً بِاللَّهِ مِنَ النَّارِ .

"Amesikia msikilizaji kusifiwa kwa Mwenyezi Mungu, na uzuri wa neema zake juu yetu. Mola wetu kuwa nasi na tufadhilishe, hali ya kuwa tunajilinda na Mwenyezi Mungu kutokana na moto."

**104. Dua ya msafiri akishuka sehemu wakati yuko safarini.**

(٢١٦) أَعُوْذُ بِكَلِمَاتِ اللّٰهِ التَّامَّاتِ مِنْ شَرِّ مَاخَلَقَ .

"Najilinda kwa maneno ya Mwenyezi Mungu yaliyotimia na shari ya alicho kiumba."

**105. Dua ya msafiri akirudi kutoka safarini.**

*(217) Imepokewa kutoka kwa Ibn Omar (R.A) kwamba Mtume ﷺ alikuwa akirudi vitani au kutoka Hijjah katika kila akipanda mlima akisema:*

اللّٰهُ أَكْبَرُ ، اللّٰهُ أَكْبَرُ ، اللّٰهُ أَكْبَرُ .

"Mwenyezi Mungu ni Mkubwa, Mwenyezi Mungu ni Mkubwa,

Mwenyezi Mungu ni Mkubwa."

*kisha akisema:*

